# Nipashe

Jumatatu Agosti 15, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581038

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SportPesa

JACKPOT BABA LAO!

TZS. 315,715,520

CHEZA SASA KWA 1000/= TU!

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**REA** kuwadhamini mkopo wa bilioni 2/- wanaoanzisha vituo vya mafuta vijijini...

UKURASA 4



WACHEZAJI 7 EPL WANAOLIPWA FEDHA NYINGI ZAIDI 2022-23

UKURASA 12

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa



# Samia: Hiki ndicho kipaumbele changu

- **Asema** hii sio Tanzania tunayoitaka, twendeni tukajenge...TARURA yapewa jukumu... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 19

**IEBC YAFIKIA KUHAKIKI NUSU KURA, ODINGA AONEKANA KUONGOZA**

WAKATI Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya (IEBC) imefikia nusu ya...

## TFRA yatoa orodha vituo mawakala ruzuku mbolea

UKURASA 4



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza jambo na Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete katika matembezi ya kilometa tano ya CRDB Bank Marathon jijini Dar es Salaam. Wengine ni Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu (wa pili kushoto), Mke wa Makamu wa Rais, Mama Mbonimpaye Mpango (kulia), pamoja Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wachimba miamba kutafuta maji UK.2

**MICHEZO** NABI AING'ATA SIKIO SIMBA KWA ZORAN UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Baadhi ya wanawake wa Mtaa wa Kanyerere, Kata ya Butimba, Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza wakiendelea na shughuli za uchotaji maji usiku katika korongo walilochimba kwa ajili ya kujipatia maji baada ya huduma hiyo kukosekana kwa zaidi ya miezi. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Samia: Hiki ndicho kipaumbele changu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kipaumbele chake cha kwanza kwa sasa ni wananchi, ndiyo sababu ya kuongeza fedha kwenye sekta za uzalishaji ili kumgusa moja kwa moja hasa mwananchi wa hali ya chini.

Aidha, amewaonya makandarasi wababaishaji na kutaka orodha yao ifikishwe mamlaka husika ili wasipewe kazi huku akiagiza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuhakikisha mikataba 969 iliyosainiwa haiangukii mikononi mwa madalali.

Kadhalika, Rais Samia ameiongezea majukumu TARURA kuratibu miradi mingine ya miundombinu inayojengwa mijini na vijijini ikiwamo mradi wa uboreshaji miundombinu kwenye majiji (TACTIC) na mradi wa uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP).

Rais Samia alitoa maelekezo hayo jana jijini hapo kwenye hafla ya kusaini mikataba 969 yenye thamani ya Sh. bilioni 331.39 ya ujenzi wa barabara zinazosimamiwa na TARURA kwa mwaka 2022/23.

Alisema barabara hizo zikiimarishwa zitaboresha maisha ya Watanzania kwa kuwa zinaunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko.

"Hatusemi tunaacha vipaumbele vya kitaifa huko, hapana ila kipaumbele cha kwanza ni mwananchi kule chini twendeni tukawajengee miundombinu."

"Kwanini tumefikiria hivyo, wakati tunaenda kwenye kampeni 2020 maeneo kadhaa tulikuwa tunaambiwa daraja lilivunjika, lakini mengine yamejengwa kwenye viwango ambavyo haviridhishi limeenda kubumbwabumbwa daraja hapo, mvua moja daraja limebomoka, watoto wanashindwa kwenda shule wajawazito wanakufa njiani tumeyakuta."

"Na niliona kwenye TV maeneo mengine ya mito watu wanashindwa kutoka, vijana wanajiajiri wana matenki (matangi), mtu anatumbukizwa kwenye tenki (tangi) kisha linasukumwa hadi upande wa pili unalipa fedha za watu kama ni Sh. 1,000 au 2,000, sasa binadamu ukamtie kwenye tenki umfunike akifika amekufa? Hii sio Tanzania tunayoitaka, twendeni tukajenge madaraja watu wavuke, kazi iendelee," alisema.

Kuhusu makandarasi wababaishaji alimwagiza Mtendaji Mkuu wa TARURA awasilishe kwa Bodi ya Usajili ya Makandarasi na Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) orodha ya makandarasi walio onesha ubabaishaji ili wasipewe tena kazi maeneo mengine na kuendelea kuharibu.

"TARURA isiingie makubaliano na makandarasi yeyote kabla ya kujiridhisha uwezo wa kutimiza makubaliano ya mkataba wa ukandarasi, utoaji zabuni na tathmini zake uzingatie sheria ya manunuzi ya umma, kanuni pamoja upekuzi wa kupata makandarasi wenye uwezo," alisema.

Kadhalika, alitaka mikataba hiyo iliyosainiwa kutokwenda mikononi mwa madalali bali iende kwa makandarasi wenye uwezo na vigezo stahiki.

"Wengine wanaopewa hawafahamu kazi zenyewe na wengine huomba kazi nyingi au kubwa kuliko uwezo walionao kivifaa na kitaalamu na kushindikana kabisa jambo linaloleta migogoro kwa TARURA."

"Naomba mkatimize wajibu wenu kama mikataba yenu mliyosaini inavyosema kwa wakati, thamani ya fedha na viwango vya yale mnayoenda kujenga," alisema.

Pia aliwataka watendaji wa wakala huo kujiepusha na mgongano wa maslahi kwenye taratibu za manunuzi.

"Bwana Seff (Mtendaji wa TARURA) wewe ndio msimamizi mkuu hapa kajipekue humo ndani, je, wote tunakwenda njia moja au waliowekwa wanafanya kazi inayotakiwa," alisema.

Alitaka TARURA kuwa na mipango ya muda mfupi na mrefu na taratibu zote za kuanzisha miradi zianze mapema na kwa uwazi ili kuepuka migongano ya kimaslahi.

Alisema utekelezaji wa maagizo hayo yatakuwa ni kipimo cha wakala huo kuongezewa fedha za kutimiza majukumu yake.

"Mnaweza kutenga bajeti nyingi kama tulivyotenga, lakini TARURA ikashindwa kuzitumia kwa hiyo niwaombe sana ili kuongeza fedha mwakani, za mwaka huu zikafanyiwe kazi vizuri, inapofika Juni mwakani barabara zote ziwe zimejengwa kila barabara ikamilike kwa wakati, wananchi wanashida sana," alisema.

Kuhusu teknolojia mbadala ya kujenga barabara, Rais Samia alisema; "nilishatoa maelekezo kwa TARURA kutumia teknolojia mbadala ili kuboresha barabara za vijijini na kuondokana na mchanga na changarawe."

Alisema mabilioni ya fedha yalikuwa yakitengwa kila mwaka yanaingizwa kwenye barabara ambazo zinaharibika hususan kila msimu wa mvua wakati kuna teknolojia ya kuzifanya ziishi kwa miaka 10 hadi 15.

Vilevile, Rais Samia aliutaka wakala huo kuratibu miradi ya TACTIC na DMDP kutokana na baadhi ya maeneo nchini kuleta matokeo yasiyotarajiwa.

"Mfano mzuri Dar es Salaam mradi wa DMDP utekelezaji ni asilimia 50 ukiuliza fedha unaambiwa zimekwisha, naomba mfanye tathmini na muisimamie," alisema.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema baada kusaini mikataba hiyo makandarasi watatakiwa kwenda maeneo ya mradi haraka na kuto tozo ya huduma na kodi zingine.

Naye Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema wizara yake haitakuwa kikwazo kutoa fedha za kutekeleza miradi na kusisitiza kufuatilia utekelezaji ili thamani ya fedha ionekane.

Awali, Mtendaji Mkuu wa TARURA, Mhandisi Victor Seff, alisema lengo la mwaka huu wa fedha ni kufanya matengenezo ya kawaida ya kilometa 21,595, barabara za lami zenye urefu wa kilomita 422, kilomita 11,074 za changarawe na madaraja 269.

Alisema kwa mwaka 2022/23, zabuni 1,706 zenye thamani ya Sh. bilioni 621 zimepangwa kutangazwa, katika awamu ya kwanza TARURA imetangaza zabuni 1,085 zenye thamani ya Sh. bilioni 378.56 sawa na asilimia 60 ya fedha zilizopangwa huku zabuni 117 zenye thamani ya Sh. bilioni 47.17 zimerudiwa kutangazwa kutokana na kukosekana kwa makandarasi wenye sifa maeneo hayo.

# Walazimika kuchimba miamba kutafuta maji

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KASI ya uharibifu wa mazingira nchini na duniani imeendelea kuleta athari kwa binadamu hali inayosababisha Jiji la Mwanza kukabiliwa na mgawo wa maji.

Moja ya eneo ambalo wananchi wake wamejikuta kwenye hali mbaya ni Mtaa wa Kanyerere, Kata ya Butimba wilayani Nyamagana, umbali wa kilomita tisa kutoka katikati ya jiji hilo.

Hali hiyo imesababisha baadhi ya wananchi kulazimika kuchimba mashimo chini ya miamba ili kutafuta maji ya kutumia nyumbani kutokana na uhaba wa huduma hiyo unaoendelea kutikisa maeneo mbalimbali.

Nipashe ilitembelea mtaa wa Kanyere ulioko katika Kata ya Butimba, wilayani Nyamagana na kuzungumza na wananchi wa eneo hilo ambao walisema wanalazimika kuamka saa nane usiku ili kuwahi foleni ya kuchota maji eneo hilo.

Adelaida Thobias, mkazi wa Mtaa wa Kanyerere alisema, kwa takribani miezi miwili wana mgawo mkali wa maji ambao hata hivyo hayatoshelezi mahitaji na kulazimika kwenda kwenye mapango ya mawe kutafuta.

Alisema wana miundombinu yote na awali walikuwa wanapata maji kila siku, lakini kadri siku zinavyosogea kiwango kinapungua na kukosekana kabisa, hali inayowalazimu kutafuta mbinu mbadala.

"Ni zaidi ya miezi miwili sasa maji hayafiki mtaani kwetu tukaamua kuchimba shimo katika mapango ili kujipatia maji, hata hivyo bado tunakumbana na adha kubwa kwani pango lenyewe ni dogo halikidhi mahitaji ya wakazi wa hapa," alisema Adelaida.

Naye Venata Venastus alisema wanapata shida ya maji licha kuwapo mabomba na kuomba utaratibu ufanyike ili wapate huduma hiyo kwa uhakika.

Alisema tatizo hilo halipo kwa wanawake pekee, hata baadhi ya wanaume wanalazimika kuchota maji katika mapango hayo mapema kabla ya muda wa kwenda kazini.

"Tunapoteza muda mwingi katika kutafuta huduma hii ya maji mpaka kuna wakati tunaacha kufanya majukumu yetu ya kimaendeleo," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kanyerere, Kansola Kamboli, alipozungumza na Nipashe mwishoni wa wiki, alithibitisha kuwapo kwa tatizo la maji katika mtaa huo.

Alisema walipata taarifa kuwa kutakuwa na mgawo wa maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), lakini mtaani kwake yamekatwa kwa muda mrefu.

"Tuliambiwa kutakuwa na mgawo wa maji ili kusaidia wateja kugawana kidogo yaliyopo, lakini mtaani kwetu hata hayo ya mgawo hatupati tumejaribu kufuatilia bado hayatoki, ndipo wananchi wakaamua kuchimba maji yao kwenye mapango," alisema.

Hivi karibuni, akizungumza na watumishi wa serikali, wanasiasa na viongozi wa dini jijini Mwanza, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso alithibitisha kuwapo kwa tatizo hilo huku akiwataka wananchi kuwa watulivu.

"Mitambo ya usambazaji wa maji iliyopo inatakiwa kusambaza jumla ya lita milioni 90, lakini kwa sasa inasambaza lita milioni 80 hivyo kuna upungufu wa lita milioni 10, tunawaomba wananchi kuendelea kuwa wavumilivu tunaposhughulikia tatizo," alibainisha.

Kwa mujibu wa waziri huyo, maeneo ya milimani ndiyo yatakumbwa zaidi na tatizo la maji yakiwamo ya Kangale A, Bulola, Mhandu, Kanyerere, Kakebe, Fumagila, Whanima, PPF Kiseke, Green View, Buguku, Igombe, Isamilo juu, Nghwashi na Luchelele Shadi.

Aliiagiza MWAUWASA kufanya mgawo huo kwa utaratibu rafiki ili wananchi wapate huduma hiyo.

Alipoulizwa kuhusu malalamiko ya wananchi hao, Ofisa Habari wa MWAUWASA, Mohamed Seif, alisema Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo yupo kikaoni na kumtaka mwandishi kumtafuta siku nyingine.

Alipopigiwa simu Mkurugenzi huyo alisema suala hilo litafafanuliwa kwenye mkutano na waandishi wa habari, ingawa hakutaja tarehe wala muda.

Maeneo mbalimbali ya Jiji la Mwanza yanakabiliwa na mgawo wa maji kutokana na mashine mojawapo katika mtambo wa kusukuma maji kuungua, huku MWAUWASA ikiwaeleza wananchi kuwa wameagiza mtambo mpya nje ya nchi.

Pia walisema hitilafu hiyo imesababisha wananchi wa maeneo ya milimani kukosa maji kwa kuwa hakuna mashine ya kuyasukuma kwa kasi.



Maofisa mradi wa kielektroniki wa Hakiki Stempu (ETS) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ruekaza Rwegoshora (kushoto), Lewis Rwenyagira na mabalozi wa mradi huo, wakionyesha kwa waandishi wa habari mfumo wa kuhakiki stempu kielektroniki unavyofanyakazi katika maonyesho ya Nanenane yaliyomalizika hivi karibuni, jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rutinwa awataka wa-TZ kupenda kusoma vitabu

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Bonaventure Rutinwa, amesema sekta ya usomaji vitabu ni muhimu katika kujenga kizazi chenye kupenda kusoma na kutoa wito kwa wazazi kuhakikisha wanawapatia vitabu vya kusoma ili wapate maarifa.

Prof. Rutinwa aliyasema hayo jana katika hafla ya kuzindua kitabu kipya cha watoto kinachojulikana kama The African Alphabet jijini Dar es Salaam jana.

Kitabu hicho kimeandikwa na Kemilembe Mugangala, ambaye ni mwanafunzi wa mwaka wa nne katika Chuo Kikuu cha Drake nchini Marekani, anayesomea fani ya utengenezaji wa vipindi kwa mfumo wa kidigitali (digital media production).

Kitabu hicho kimelenga kufundisha watoto wa madarasa ya awali herufi kwa kutumia alama na majina yanayoendana na mazingira ya Kiafrika.

Aidha, alimpongeza Mugangala kwa kutunga kitabu hicho kwa lugha nyepesi inayoweza kueleweka kwa watoto sambamba na kuzingatia kuwezesha watoto kuelewa utamaduni na mazingira ya Kitanzania na Kiafrika.

Prof. Rutinwa alisema kutokana na mabadiliko makubwa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kuna umuhimu mkubwa wa kupambana kulinda mila na utamaduni wetu wa Kiafrika usipotee.

Mugangala alisema kilichomsukuma kuandika kitabu hicho ni uzoefu wa mazingira aliyosomea kuona watoto wanajifunza kwa kutumia vitabu vilivyoandikwa kwa utamaduni na mazingira ya nchi za Magharibi wakati Tanzania na Afrika kwa ujumla tuna tamaduni zetu.

Alitoa mfano kuwa watoto wanaweza kufundishwa kwa kutumia herufi A ni Afrika, M ni kwa Matoke, Z ni kwa Zanzibar na maneno mengine mengi yaliyopo kwenye maeneo yaliyowazunguka.

"Kama mnavyojua elimu ya awali ndio msingi wa kumjenga mtoto katika safari yake ya elimu, hivyo hatua hii ni muhimu sana watoto kupata vitabu vya kusoma vilivyoandikwa kwa lugha nyepesi kueleweka kwao, ambavyo vinaweza kuwajengea uwezo wa kujua masuala mbalimbali na kujitambua, mila na utamaduni wao," alisema Muganga.

Alisema kitabu cha The African Alphabet kinahamasisha uthamini wa mila za Kiafrika hususani katika kipindi hiki cha utandawazi ambapo wazazi wengi hawapati muda wa kutosha wa kukaa na watoto wao hali inayosababisha watoto kujifunza mila, imani na tamaduni za kigeni.

"Kutokana na maendeleo ya teknolojia ya sayansi na TEHEMA, kumekuwapo na mabadiliko ya tamaduni mbalimbali kutokana na matumizi ya internet na vifaa vya kisasa vya kielektroniki kama simu janja (smart Phones), kompyuta, luninga na mitandao ya kijamii.

Alitoa wito kwa wadau wote wa tasnia ya uandishi wa vitabu kushirikiana pamoja, kuzidi kutunga vitabu vizuri vya kusisimua, ili kufufua ari na mwamko wa Watanzania kupenda kusoma na sio kusoma tu bali kusoma vitabu vyenye kuwajengea uwezo wa kupata maarifa.

# Chongolo apongeza kasi ujenzi shule 200 nchini

**Na Steven William,** MUHEZA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema kuwa serikali imejenga shule zaidi ya 200 za sekondari nchini ili kuwawezesha watoto kupata elimu.

Akihutubia wananchi wa Kata ya Kisiwani na Kilulu wilayani Muheza mkoani Tanga, alisema serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha kila mwanafunzi anayefaulu anaendelea na kidato cha kwanza.

Alisema katika Kata ya Kisiwani imejengwa shule ya sekondari ambayo imewawezesha wanafunzi kutotembea umbali mrefu na kusoma katika mazingira mazuri.

Kwa mujibu wa Chongolo, kwa sasa atasukuma ajenda ya ujenzi wa nyumba za walimu huku akiahidi kuwa shule hiyo itajengewa nyumba nne za walimu na kwamba ni muhimu kujenga za kutosha kwenye kila shule ili wafanyakazi wawe na uhakika na mahali pa kuishi.

Aidha, alisema elimu bure ni msaada kwa wazazi wasiojiweza na kwamba serikali inataka kila mtoto apate elimu bora kwa manufaa yake na taifa kwa ujumla.

# Baba matatani tuhuma za kumchoma mwanawe moto

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKAZI wa Kitongoji cha Darpoli Kijiji cha Lunyele, Martin Emmanuel (25), anashikiliwa na polisi mkoani Ruvuma, kwa tuhuma za kummwagia mafuta ya petroli na kumchoma moto mtoto wake wa kufikia mwenye umri wa miaka mitano kwa maelekezo ya mganga wa jadi ili apate utajiri.

Mtoto huyo (jina linahifadhiwa) ni mwanafunzi wa darasa la awali ambaye amejeruhiwa sehemu kubwa ya mwili wake na anaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Mbinga.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi mkoani Ruvuma, Pilli Mande, alisema tukio hilo lilitokea Agosti 9, mwaka huu, majira ya saa 10 jioni.

Akielezea tukio hilo, Kamanda Pilli alisema, siku ya tukio baba huyo alimchapa mtoto huyo na kummwagia mafuta ya petroli mwili mzima na kumuwasha moto.

Kamanda Pilli alisema, kitendo hicho kilisababisha mtoto huyo alie kwa mauvimu makali aliyokuwa akiyapata hali iliyofanya majirani wafike kumsaidia kuuzima moto huo na kumpeleka hospitalini.

Alisema mtoto huyo anaendelea na matibabu na hali yake ni mbaya kutokana na moto kumuunguza sehemu kubwa ya mwili wake.

Mande alisema uchunguzi wa awali wa polisi ulibaini baba huyo alikwenda kwa mganga kutafuta dawa za kumwezesha kuwa tajiri na kupewa sharti la kumteketeza mtoto huyo kwa moto, ndiyo maana alitenda tukio hilo la kikatili.

Aidha, alisema polisi wanaendelea na upelelezi ambao ukikamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria, huku akiwataka wananchi kutafuta utajiri kwa kufanyakazi na kutokubali kudanganywa na waganga.


**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 154 YA MWAKA 2022.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMEU PETER JOHN MOSHA**

**HYASINTA PETER MOSHA............................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu, wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 18 mwezi wa octoba, 2022.
Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 05 mwezi wa Agosti, 2022.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imtolewa leo tarehe 15/06/2022.**

NAIBU MSAJILI

**FOMU MIRATHI-2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ............TEMEKE**

**Kituo cha...... JUMUISHI.... Mkoa... DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi............1508/2022................**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ABDUL MALIK SAID HEMED**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**

**NA: TARIQ SAID HEMED**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 02 mwezi 09 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 12 mwezi 08 mwaka 2022**

HAKIMU

**FOMU MIRATHI-2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ............TEMEKE**

**Kituo cha...... JUMUISHI.... Mkoa... DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi............1507/2022................**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: SAID HEMED SALUM**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**

**NA: JUMA ABDALLAH ISMAIL**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 mwezi 08 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 12 mwezi 08 mwaka 2022**

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
13 – 08 – 2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kutaarifu umma kuwa siku ya **Jumatatu tarehe 15 – 08 – 2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji,** gari hizo zenye namba za usajili:
   **T 332 BYR / T 387 DHQ T 406 DFE / T 416 AYQ T 897 BNS / T 321 DDH T 266 BXH / T 393 DVS T 316 CZS / T 394 DVS**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **23** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.2** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.1** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

116989602




Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti (kulia), akitoa ishara ya kuzindua kampeni ya kuhamasisha utalii wa ndani kwa kupanda Mlima Kilimanjaro kwa wafanyakazi 28 wa kampuni hiyo, jana mkoani Kilimanjaro. Ikiwa ni sehemu ya programu ya kampuni hiyo kujenga afya ya mwili kwa wafanyakazi wake kwa kufanya mazoezi wakitarajiwa kushuka Agosti 20. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Moshi mweupe urais Kenya kesho

**Na Jenifer Gilla**

Moshi mweupe unatarajiwa kuonekana kesho katika anga la Kenya, ikiwa ni siku ya mwisho kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya (IEBC), kutangaza matokeo ya urais katika uchaguzi uliofanyika Agosti 9, mwaka huu.

Kwenye maeneo mbalimbali ya nchi hiyo baadhi ya wananchi wamelalamika Tume hiyo kuchukua muda mrefu kutangaza matokeo ya urais hali inayokwamisha shughuli za uzalishaji.

Akizungumza na chombo kimoja cha habari, mmoja wa wapigakura mkazi wa Uasin Gishu, Dennis Kichirichiri, alisema maduka mengi yamefungwa kwa kuwa wananchi wengi walikwenda kupiga kura maeneo waliyojiandikisha.

"Tunaomba watuharakishie (uchaguzi) shughuli hii kwa sababu kama unavyoona maduka yote yamefungwa, sasa hivi biashara ya Uasin Gishu ingekuwa inaendelea vizuri. Rais yeyote atakayechaguliwa sisi tutampokea, haya mambo yanayoendelea yatasababisha uchumi ushuke," alisema.

Mwananchi mwingine ambaye hakujitambulisha jina, alisema Kiblagachi Chimode "Kura tumeshapiga, kazi zimekwama tumesimama hatujui tufanyeje, si wamtangaze huyo rais, hapa nilipo sina unga, sina chakula, sina fedha nitapata wapi, hakuna usafiri."

Wakati hali ikiwa hivyo, juzi Tume hiyo ilisema inakuja na mpango kazi mpya utakaowezesha kazi hiyo kufanyika kwa haraka kukamilisha ujumlishaji wa kura za urais.

Mwenyekiti wa IEBC, Wafula Chebukati, alisema mpango kazi uliopo unachukua saa tatu hadi nne kwa ofisa mmoja kuhudumiwa katika kituo cha kitaifa cha uchaguzi cha ukumbi wa Bomas Nairobi.

"Tuna baadhi ya maofisa ambao wamekaa kwenye viti hivi kwa siku tatu. Maofisa 265 wameripoti. Tumefaulu kuwashughulikia 141 na kusalia na 124 ambao bado wako kwenye foleni. Wasimamizi wa uchaguzi watakabidhi fomu zao asili 34A kwa ofisa wa kitaifa wa kujumlisha baada ya tangazo hili," alisema Chebukati.

Duru za siasa nchini humo zinaeleza kuwa mchuano mkali ni baina ya Raila Odinga (Muungano wa Azimio la Umoja One Kenya maarufu kama Azimio Coalition) na William Ruto (Chama cha United Democratic Alliance (UDA), huku Ruto akiongoza kwa kupata magavana 21, maseneta 24 na wabunge 149 wakati Odinga akiwa na magavana 19, maseneta 22 na wabunge 141.

Aidha, mchuano baina ya viongozi hao ni mkali ukiwa na mpishano wa namba chache, ikilinganishwa na uchaguzi wa mwaka 2017 kati ya Odinga na Uhuru Kenyatta ambaye ameongoza taifa hilo kwa miaka 10 tangu 2013.

Wagombea wengine wa urais kwenye uchaguzi huo ni Prof. George Wajackoya wa Chama cha Roots na Waure Waohiga wa Chama cha Agano.

Tangu kuwa na mfumo wa vyama vingi nchini humo atakayeshinda nafasi hiyo atakuwa ni rais wa tano kuongoza taifa hilo.

# TFRA yataja orodha mawakala ruzuku ya mbolea

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imetoa orodha ya vituo 218 vya mawakala watakaokuwa wanatoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima katika mikoa mbalimbali nchini kuanzia leo.

Kwa mujibu wa tangazo TFRA lililochapishwa ukurasa wa saba hadi wa 10, mwaka wa fedha 2022/2023 serikali itatoa kutoa ruzuku hiyo ya mbolea kwa lengo la kuwawezesha wakulima nchini kuinunua kwa bei himilivu.

Tangazo hilo limeeleza kuwa mbolea hiyo ya ruzuku inaanza kutolewa leo katika vituo mbalimbali vya mawakala waliosajiliwa ambao watauza na kusambaza kwa wakulima.

Aidha, limeonyesha idadi ya vituo kwa kila mkoa kwenye mabano kuwa ni Dar es Salaam (3), Iringa (43), Kigoma (6), Kilimanjaro (10), Mbeya (30), Njombe (41), Ruvuma (12), Shinyanga (5), Songwe (32) na Katavi (4). Vitu vingine ni Manyara (1), Mwanza (3), Tabora (5), Arusha (3), Geita (1), Simiyu (2) na Tanga (1).

Wiki iliyopita Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani Njombe na Iringa, alisema serikali imeweka ruzuku ili kuwapunguzia makali ya bei wananchi, kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula, huku akiwataka kuzalisha kwa wingi na kutokubali kuuza chakula chote.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Tabora, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa aliwataka mawakala wote ambao wamepewa kazi ya kusambaza mbolea hiyo kuwa waaminifu na kuhakikisha inawafikia wakulima kama ambavyo imekusudiwa.

Alisema serikali haitawafumbua macho watakaohujumu ruzuku hiyo ambayo imetolewa na serikali kwa wakulima na yeyote atakayebainika kufanya hujuma atachukuliwa hatua kali.

"Serikali imetoa ruzuku hii ya mbolea kwa wakulima kwa nia nzuri kabisa, tunachoomba iwafikie wakulima na ikafanye kazi iliyokusudiwa na serikali, niwaambie tu kwamba kama kutakuwa na mtu yeyote atakayejaribu kuhujumu nia hii njema ya serikali atachukuliwa hatua kali," alisema Msigwa.

Hivi karibuni, Mkurugenzi Mtendaji TFRA, Dk. Stephan Ngailo, alisema ili kupata ruzuku hiyo wakulima watatakiwa kwenda serikali za vijiji vyao kujisajili kwa ajili ya kuingizwa kwenye mpango huo wa utoaji wa ruzuku za mbolea na kwamba kiasi cha Sh.bilioni 150 kimetengwa kwa ajili hiyo.

# REA kuwadhamini mkopo wa bil. 2/- wanaoanzisha vituo vya mafuta vijijini

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA), umesema zaidi ya Shilingi bilioni mbili zitakopeshwa kwa wananchi wanaotaka kuanzisha vituo vya kuuza mafuta vijijini ili kuhakikisha usalama wa watu na bidhaa hiyo kwa vyombo vya usafiri na mitambo.

Kwa sasa wakala huo unakamilisha taratibu za kutoa mikopo hiyo na kuwatambua waombaji, maeneo yatakayowekwa vituo na kuhakikisha tathmini ya uharibifu wa mazingira imefanyika.

Tangu kuanzishwa kwa REA mwaka 2007, zaidi ya Shilingi trilioni tatu zimetumika kusambaza nishati vijijini, pia kuchangia ukuaji wa uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na maendeleo vijijini kwa asilimia 25.

Hayo yalisemwa na mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Saidi na Mkurugenzi wa Uendeshaji Masoko na Teknolojia, Advera Mwijage, wakati wakizungumzia majukumu, changamoto na mafanikio ya wakala tangu kuanzishwa kwake.

Advera alisema, wamefikia uamuzi huo kutokana na mwenendo holela wa uuzaji mafuta vijijini na hatarishi kwa maisha ya watu, kuharibu vyombo vya usafiri na kwamba utaratibu utakaotumika ni kuwaunganisha na benki ziwakopeshe.

"Wengi wanaweka mafuta kwenye magaloni na kuhifadhi ndani ya nyumba ambako ni hatari ikiwa yatalipuka, lakini usafi wa bidhaa hiyo ni changamoto, tunawataka wananchi wauze mafuta kwa utaratibu mzuri na usafi ndiyo maana tumekuja na mikopo hii ambayo tutawadhamini kwa mwaka huu wa fedha," alisema.

Alisema utafiti uliofanywa na REA mwaka 2017 ulibaini kuna visiwa 196 nchini, kati yake 53 havina makazi ya kudumu, 143 vina watu na kati yake 72 vina nishati na 71 havina ya uhakika.

"Moja ya jukumu la REA ni kutoa ufadhili kwa kampuni au mtu binafsi anayetaka kuwekeza kwenye nishati jadidifu kwa kuchangia asilimia 25 na serikali 75, tumevifikia visiwa 38 kwa umeme wa jua na upepo ambavyo vinakaliwa na watu kati ya 50 hadi 70, tunaendelea na mpango wa kuweka nishati kila vijiji vyenye watu wengi," alifafanua.

Alisema nishati vijijini ni muhimu kwa maendeleo ya watu na utafiti unaonyesha kuwa asilimia 65.5 ya Watanzania wanatumia kuni kwa ajili ya nishati, asilimia 26.2 wanatumia mkaa, asilimia 5.1 gesi na asilimia tatu, umeme.

Advera alisema kwa ujumla asilimia 84.6 ya kaya zote vijijini zinatumia kuni kupata nishati, huku akisisitiza umuhimu wa kuhakikisha nishati ya kupikia inapatikana kutokana na kasi ya mabadiliko ya tabianchi.

Mkurugenzi Said alisema REA imefanikiwa kuchochea maendeleo vijijini kwa watu kutambua fursa zilizopelekwa na nishati, kwa kufungua karakana za kutengeneza vifaa vya ujenzi, saluni za kiume na kike na mahitaji mengine ambayo zamani ilikuwa lazima wayafuate mjini.

Alisema kwa sasa kasi ya vijana kurudi vijijini kufungua maeneo ya biashara ambazo zinachagizwa na umeme ni kubwa na REA inaendelea kuwasaidia lengo ni kuchagiza maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Majukumu ya REA ni kuboresha maisha ya watu vijijini, kuchochea ukuaji wa uchumi, kuboresha huduma za kijamii kama afya, maji na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kuhifadhi mazingira na kuimarisha usawa wa kijinsia," alisema.

Said alisema, tangu kuanzishwa kwa REA zimetumika zaidi ya Shilingi trilioni tatu kufikisha umeme vijijini na hiyo inaendelea kwenye vitongoji vyote nchini.

"Kuna utafiti ulionyesha kuwa vifo vinavyotokea Afrika 33,000 ni magonjwa ya mfumo wa kupumua ambayo yanasababishwa na kuathirika kwa mapafu kwasababu ya moshi wa kuni na wengi ni wanawake na wasichana, ndiyo maana tumeongeza kasi ya kusambaza nishati, ingawa kwenye nishati ya kupikia bado hatujawafikia wengi," alisema mkurugenzi huyo.

HABARI KITAIFA

# Vijana 240 kuwezeshwa kujiajiri sekta ya mifugo

**Na Mbaraka Kambona,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (pichani), amesema kuanzia mwaka huu wa fedha 2022/23 wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) na Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA), imeanzisha vituo atamizi nane ambavyo vitahusisha vijana 240 waliohitimu taaluma za mifugo kwa ajili ya unenepeshaji mifugo katika vituo vya mikoa ya Tanga, Kagera, Songwe na Mwanza.



Waziri Ndaki alisema hayo jijini Dodoma mwishoni mwa wiki katika taarifa yake kwa umma kuhusu utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa kwenye kilele cha maadhimisho ya sherehe za Wakulima (Nanenane) yaliyofanyika jijini Mbeya Agosti 8, 2022.

"Nimeziagiza taasisi hizo kuanza ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya unenepeshaji wa mifugo mara moja na kukamilisha taratibu za kuwapatia vijana," alisema Ndaki.

Alisema kuwa ili kufanikisha hilo, wizara itashirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wahitimu wajasiriamali wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), wanaofahamika kama SUGECO, Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Benki ya CRDB, Viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo nchini, Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Taasisi ya Dhamana ya Uwezeshaji Kilimo (PASS) na NARCO.

Vile vile, baada ya kupitia mikataba na mipango ya kibiashara kwa kila mwekezaji katika vitalu vya NARCO watatenga unenepeshaji wa mifugo kwa ajili ya kuwapangisha vijana hao watakaohitimu katika vituo hivyo atamizi.

Kuhusu tathmini ya upangishaji wa vitalu vya NARCO, Ndaki alisema kuwa wizara imeunda timu ya wataalamu kutoka serikalini na taasisi mbalimbali za sekta binafsi kufanya tathmini ya kina ya utendaji na changamoto zinazoikabili kampuni hiyo ili waweze kuishauri vizuri serikali.

Alisema kuwa NARCO inafanya mapitio ya mikataba na mipango ya biashara kwa kila mwekezaji kulingana na mikataba yao ili kubaini hali halisi ya uwekezaji.

Ili uwekezaji wenye tija katika Ranchi za NARCO uweze kufanyika kikamilifu, Waziri Ndaki alisema NARCO imeainisha na kutenga vitalu vitano vyenye ukubwa wa takriban hekta 32,500 ili kuvutia wawekezaji mahiri na wenye mitaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Agosti 8, 2022 akiwa jijini Mbeya, Rais Samia Suluhu Hassan aliitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ili kuwawezesha vijana kujiajiri katika sekta ya mifugo na kufanya maboresho makubwa ya utendaji wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO).

# Wakulima wapata neema mikopo ya trekta Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), tawi la Shinyanga, imetoa mkopo wa matrekta mawili kwa wakulima ili kuunga juhudi za serikali za kukuza sekta ya kilimo na uchumi wa taifa.

Matrekta hayo yalikabidhiwa juzi na mjini hapa na Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko katika hafla iliyohudhuriwa na maofisa wa kampuni ya usambazaji wa zana za kilimo Agricom.

Meneja wa NBC tawi la Shinyanga, Joyce Chagonja, akizungumza wakati wa hafla hiyo ya kukabidhi matrekta kwa wakulima, alisema wana fursa nyingi za mikopo kwa ajili ya mkulima, ikiwamo kuwakopesha zana za kilimo, pamoja na bima za mazao.

Alisema ukopeshaji wa matrekta hayo hauna masharti magumu, anachotakiwa mkulima kuwa na shamba lake binafsi na katika mkopo huo atachangia asilimia 25, huku wao wakichangia asilimia 75 na marejesho yake ni nafuu hayamsumbui mkopaji.

"Matrekta ambayo tumekabidhi kwa wakulima hawa gharama zake ni Sh. milioni 40.7 kwa kila trekta na wakulima wamechangia asilimia 25 ya fedha," alisema Chagonja.

"Benki ya NBC tupo pamoja na serikali kukuza sekta ya kilimo kwa sababu tunatambua kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo, kinachukua asilimia 80 ndiyo maana tumekabidhi zana hizi za kilimo kwa wakulima," aliongeza.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, aliipongeza benki hiyo kwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kukuza sekta ya kilimo.

Aidha, aliipongeza kwa kutoa mikopo ya zana za kilimo kwa wakulima, huku akitoa wito kwa kuzitumia kufanya kilimo chenye tija na kuongeza kasi ya uzalishaji wa mazao.

Golea Kamata, aliyepata mkopo huo alisema, zana hizo za kilimo zitakuwa chachu ya mabadiliko na kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla kupitia sekta ya kilimo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

LATRA

## TAARIFA KWA UMMA

### MIKUTANO YA KUKUSANYA MAONI KUHUSU VIWANGO VYA NAULI ZA TRENI KWA MIKOA YA DAR ES SALAAM, KIGOMA NA MWANZA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imepokea maombi kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC) ikiomba ongezeko la nauli kwa asilimia 15 kwa abiria wanaotumia usafiri wa treni Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria Na. 3 ya LATRA, 2019 Mamlaka inapaswa kukusanya maoni ya wadau kabla ya kufikia uamuzi wa kuridhia viwango vya nauli kwa huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka ikiwemo nauli za treni.

Katika kulitekeleza hilo, Mamlaka imeandaa mkutano wa kupokea maoni ya wadau wa usafirishaji, ikiwa ni pamoja na watoa huduma, watumiaji wa huduma na wananchi kwa ujumla.

Mikutano hiyo itafanyika **tarehe 19, 22 na 24 Agosti 2022 saa nne kamili asubuhi (4:00),** kwa Dar es salaam (Ukumbi wa Anatorglo) Kigoma (Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa) na Mwanza (Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa) mtawalia.

**Nauli zinazopendekezwa na TRC ni Kama ifuatavyo:**

Jedwali Na. 1. Nauli za treni ya abiria ya 'Deluxe' kutoka Dar es salaam

| Vituo | Umbali | Daraja la pili-kulala | | Daraja la pili-kukaa | | Daraja la tatu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Km | Nauli ya zamani | Nauli Pendekezwa | Nauli ya zamani | Nauli Pendekezwa | Nauli ya zamani | Nauli Pendekezwa |
| Ruvu | 79 | 13,800 | 15,800 | 8,300 | 9,500 | 5,800 | 6,700 |
| Wami | 151 | 18,000 | 20,700 | 10,800 | 12,400 | 7,600 | 8,700 |
| Morogoro | 202 | 21,200 | 24,300 | 12,700 | 14,600 | 8,900 | 10,300 |
| Mkalamo | 203 | 21,200 | 24,300 | 12,700 | 14,600 | 8,900 | 10,300 |
| Kilosa | 289 | 25,400 | 29,200 | 15,300 | 17,500 | 10,700 | 12,300 |
| Korogwe | 291 | 25,400 | 29,200 | 15,300 | 17,500 | 10,700 | 12,300 |
| Mombo | 335 | 27,500 | 31,600 | 16,500 | 19,000 | 11,600 | 13,300 |
| Dodoma | 465 | 34,900 | 40,100 | 21,000 | 24,100 | 14,700 | 16,900 |
| Same | 459 | 33,800 | 38,900 | 20,300 | 23,400 | 14,200 | 16,400 |
| Moshi | 558 | 39,100 | 45,000 | 23,500 | 27,000 | 16,500 | 18,900 |
| Arusha | 644 | 44,400 | 51,000 | 26,700 | 30,600 | 18,700 | 21,500 |
| Tabora | 850 | 54,900 | 63,200 | 33,000 | 37,900 | 23,100 | 26,600 |
| Urambo | 940 | 59,200 | 68,000 | 35,500 | 40,800 | 24,900 | 28,600 |
| Kigoma | 1,254 | 76,100 | 87,500 | 45,700 | 52,500 | 32,000 | 36,800 |

Jedwali Na. 2. Nauli za treni ya abiria daraja kawaida kutoka Dar es salaam

| Vituo | Umbali KM | Daraja la Kwanza | | Daraja la Pili | | Daraja la Tatu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Nauli ya zamani | Nauli Pendekezwa | Nauli zamani | Nauli Pendekezwa | Nauli zamani | Nauli Pendekezwa |
| Pugu | 20 | 12,200 | 14,000 | 10,600 | 12,100 | 6,100 | 7,000 |
| Ngerengere | 144 | 20,700 | 23,800 | 16,600 | 19,100 | 9,000 | 10,300 |
| Morogoro | 202 | 24,300 | 28,000 | 19,200 | 22,000 | 10,200 | 11,800 |
| Kimamba | 271 | 28,000 | 32,200 | 21,700 | 25,000 | 11,500 | 13,200 |
| Kilosa | 289 | 29,200 | 33,600 | 22,600 | 26,000 | 11,900 | 13,700 |
| Dodoma | 465 | 40,100 | 46,100 | 30,300 | 34,900 | 15,600 | 18,000 |
| Manyoni | 595 | 47,400 | 54,500 | 35,500 | 40,800 | 18,100 | 20,800 |
| Itigi | 635 | 49,800 | 57,300 | 37,200 | 42,800 | 18,900 | 21,800 |
| Tabora | 850 | 63,200 | 72,600 | 46,700 | 53,700 | 23,500 | 27,000 |
| Kaliua | 973 | 70,500 | 81,000 | 51,800 | 59,600 | 26,000 | 29,900 |
| Isaka | 982 | 71,700 | 82,400 | 52,700 | 60,600 | 26,400 | 30,300 |
| Uvinza | 1,141 | 81,400 | 93,600 | 59,600 | 68,500 | 29,700 | 34,100 |
| Shinyanga | 1,045 | 75,300 | 86,600 | 55,300 | 63,600 | 27,600 | 31,800 |
| Mto Ugalla | 1,083 | 77,700 | 89,400 | 57,000 | 65,500 | 28,500 | 32,700 |
| Katumba | 1,149 | 81,400 | 93,600 | 59,600 | 68,500 | 29,700 | 34,100 |
| Mpanda | 1,183 | 83,800 | 96,400 | 61,300 | 70,500 | 30,500 | 35,100 |
| Mwanza | 1,229 | 86,200 | 99,200 | 63,000 | 72,500 | 31,400 | 36,000 |
| Kigoma | 1,254 | 87,500 | 100,600 | 63,900 | 73,500 | 31,800 | 36,500 |
| Nauli zinazopendekezwa zitawasilishwa kwa ufafanuzi zaidi wakati wa mkutano husika | | | | | | | |

Kutokana na umuhimu wa mkutano huo, LATRA inawaalika wadau wa sekta ya reli na wananchi kwa ujumla kushiriki bila kukosa katika mkutano kama ilivyoelezwa hapo juu.

LATRA pia itapokea maoni kwa maandishi. Maoni hayo yawasilishwe katika Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu, S.L.P. 3093, Dar es Salaam, iliyopo katika Jengo la Mamlaka, Barabara ya Nkrumah kabla ya **tarehe 31 Agosti, 2022.** Aidha, maoni ya wadau yanaweza kutumwa kwa barua pepe kupitia anuani hizi: **info@latra.go.tz** na **dg@latra.go.tz .**

**Imetolewa na:**

J. J. Kahatano

**Kny: Mkurugenzi Mkuu,**
**9 Agosti, 2022**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

Jengo la LATRA Makao Makuu, Mtaa wa Nkrumah 454/160, S. L. P. 3093, Dar es Salaam
Simu + 255 222 197 500/2, Nukushi: + 255 222 116 697
Barua pepe: dg@latra.go.tz , info@latra.go.tz , Tovuti: www.latra.go.tz

216984902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Karibu Ligi Kuu 2022/23, waamuzi tendeni haki

**UTEPE** wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2022/23, unatarajiwa kukatwa rasmi leo baada ya msimu mpya kuzinduliwa mwishoni mwa juma kwa kuchezwa mechi ya Ngao ya Jamii kati ya wakongwe wa soka nchini, Simba na Yanga.

Mechi hiyo, ambayo huwa maalum kwa kukaribisha msimu mpya, Yanga iliibuka na ushindi wa mabo 2-1, hivyo kuelekea kuanza msimu mpya vizuri wakati huu ikijiandaa sasa kucheza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Bara 2022/23 kesho itakaposhuka Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arsusha kuwakabili wenyeji, Polisi Tanzania.

Mchezo huo utafuata baada ya mechi mbili za kwanza za Ligi Kuu msimu huu zitakapopigwa leo wakati Ihefu FC ya Mbarali mkoani Mbeya itakapofungua pazi la ligi hiyo kwa kuikaribisha Ruvu Shooting huku Namungo FC ya Lindi nayo ikiwa mwenyeji wa Mtibwa Sugar kutoka Morogoro. Aidha, mbali na mechi ya Polisi Tanzania dhidi ya Yanga kesho, pia siku hiyo hiyo kutapigwa michezo mingine miwili ambapo Singida Big Stars ya mjini Singida itakuwa mwenyeji wa Tanzania Prisons wakati Dodoma Jiji FC, ikiikaribisha Mbeya City.

Mzunguko wa kwanza wa Ligi hiyo utakamilika keshokutwa, Jumatano kwa kupigwa mechi tatu ambapo Coastal Union ya Tanga itaikaribisha KMC FC ya Dar es Salaam huku Simba ikiwa mwenyeji wa Geita Gold FC katika Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati Azam FC ikiialika Kagera Sugar kwenye dimba lao la Azam Complex, Chamazi.

Kwa ujumla, tunatarajia kuona ligi bora na yenye ushindani mkubwa zaidi tofauti na msimu uliopita, hiyo ikitokana na namna tulivyoshuhudia timu zikijipanga vizuri kuanzia usajili hadi maandalizi ziliyofanya kila moja kwa wakati wake.

Si hilo tu, pia tunaamini timu nyingi zitakuwa zimetambua kwamba biashara ni asubuhi kwa kutofanya makosa katika raundi hii ya kwanza kwani ya pili huwa ni ngumu kutokana na ukweli kwamba timu nyingi hupigana kufa kupona zikitaka kujiokoa kushuka daraja wakati pia zipo ambazo huwania pointi muhimu ili kutwaa ubingwa na zile zingine zikiwania nafasi nne za juu. Msimu uliomalizika tuliona namna karibu timu 14 za Ligi Kuu zilivyokuwa zikibadilishana nafasi kutokana na kupishana pointi moja hadi tatu tu, hivyo tunatarajia kuona ushindani wa kusaka pointi tatu ukianza mapema raundi hii ya kwanza na si kusubiri hadi lala salama ya ligi hiyo.

Hata hivyo, wakati tukitarajia leo kuanza kushuhudia burudani hiyo na ushindani huo mkubwa, ni wakati sasa kwa waamuzi kuacha ubora wa timu uamue matokeo uwanjani kwa kufuata sheria 17 zinazoongoza mchezo wa soka duniani. Tunaamini wakati timu zilipokuwa zikijiandaa na msimu mpya, pia waamuzi nao walipitia vema sheria hizo 17 za soka na kusahihisha makosa yao, lakini walipigwa msasa katika kukumbushana mabadiliko mbalimbali kwenye sheria hizo ili kwenda na wakati.

Hatutarajii kuona tena makosa ya wazi kwa waamuzi yakijirudia, kwani kwa kufanya hivyo si tu watazinyonga baadhi ya timu kupata pointi zilizostahili, bali pia watawakatisha tamaa mashabiki kuendelea kuupenda mchezo wa soka na kutohudhuria kwa wingi uwanjani.

Ikumbukwe pia usajili uliofanywa na klabu zetu hapa nchini msimu huu, umegusa mataifa mengi si barani Afrika pekee bali Ulaya, Asia na hata Amerika Kusini, hivyo ni wazi mataifa kutoka mabara hayo ambayo nyota wao wanacheza soka hapa Tanzania, yatakuwa yakitupia jicho ligi yetu kwa karibu kuona kile ambacho wachezaji wao wanakifanya.


Kwa kutambua hilo, endapo waamuzi hawatazingatia sheria 17 za soka ipasavyo, si tu kwamba watazinyonga timu zilizostahili ushindi na kuwakwaza mashabiki wa ndani bali wa nje pia, lakini watazidi kujishusha thamani zao na kutopata nafasi ya kwenda kuchezesha mechi kubwa za kimataifa zenye maslahi makubwa kwao.

Tunataka kuona ligi yetu ikiwa moja ya ligi bora kabisa barani Afrika na duniani kwa ujumla ili kuvutia wawekezaji wakubwa zaidi, hivyo pamoja na mambo mengi yanayohitajika ili kufikia lengo hilo, haliwezi kutimia kama tutakuwa na waamuzi wabovu wasiozingatia sheria 17 za mchezo huo pendwa duniani. Ni wakati sasa kwa Chama cha Waamuzi nchini (FRAT) kwa kushirikiana na Bodi ya Ligi (TPLB) chini ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuhakikisha adhabu kali zaidi zinachukuliwa kwa waamuzi watakapoboronga katika majukumu yao ili kuwa fundisho na kuwarejesha walio salia katika mstari sahihi wa maamuzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera TPLB kuruhusu 12 wote kucheza Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

**SASA** imefika wakati mchezaji mwenye uwezo, mwenye nidhamu na anayejituma ndiye atakayecheza mechi. Hii ni baada ya Bodi ya Ligi nchini (TPLB), kuruhusu kutumika kwa wachezaji wote 12 wa kigeni kwa mechi moja.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari ya Mawasiliano ya Bodi ya Ligi, imesema, hilo limepitishwa na Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), katika kikao ilichoketi Agosti 9, mwaka huu jijini Arusha, ambapo kimepitia maboresho ya kanuni za Ligi Kuu, ambayo wadau wengi walipendekeza kipengele hicho.

Kabla ya maboresho hayo, klabu zilikuwa zinaruhusiwa kusajili wachezaji wa kigeni wasiozidi 12, lakini ziliruhusiwa kutumia wachezaji wanane katika mchezo mmoja.

Hiki kilikuwa ni kilio cha muda mrefu kwa wadau wa soka ambao walikuwa wanahoji ni kwa nini klabu ziruhusiwe kusajili wachezaji 12, lakini ni wanane tu waruhusiwe kwa mechi moja.

Yaani klabu inasajili wachezaji, inawalipia vibali vya kufanya kazi na pia vya kuishi nchini, lakini kwenye kila mechi ni lazima wanne wakae jukwaani, ni kanuni ambayo ilikuwa haitendi haki na ikizipotezea klabu pesa nyingi bila sababu yoyote. Kama ingeendelea ingekuwa haina maana, badala yake ni bora klabu zingeruhusiwa kusajili wachezaji wageni ambao idadi yake inaruhusiwa kuwatumia.

Ina maana klabu zingepunguziwa wachezaji kutoka 12 hadi nane, au kuacha wote watumike. Kabla ya kanuni hiyo kupitishwa, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alibainisha kuwa wanakwenda kupitisha kanuni ambazo ni rafiki kwa wadau na ambazo wengi wamezipendekeza.

Nitoe pongezi kwa TFF, TPLB na kamati yake kwa kusikiliza maoni ya wadau wengi wa soka ambao walikuwa wakilianglia hili kwa jicho la tatu. Baadhi waliona kwamba litawanyima fursa wachezaji wa kizawa ambao watakosa namba kwenye vikosi mbalimbali kwenye klabu zao.

Hawa ndiyo wanataka wachezaji wa Kitanzania wawe na upendeleo maalum hata kama hawana uwezo mzuri na wageni wabanwe, licha ya kwamba wana uwezo.

Kwa hili lililopitishwa, kwa maoni yangu, siyo kwamba litawaumiza wachezaji wa Kitanzania, la hasha. Kilichofanyika ni kwamba kila mchezaji, awe wa Kitanzania au mgeni acheze kulingana na uwezo wake na si kanuni imbebe.

Hapa ni kwamba Mtanzania anatakiwa ajitume ili apate namba na si kusubiri wageni wapunguzwe na kanuni ili yeye acheze.

Sidhani kama kuna kocha yeyote atakuwa akiwaweka tu uwanjani wachezaji 11 wa kigeni na mmoja nje kwa sababu wanatoka nje ya nchi, hapana. Makocha watakuwa wanapanga timu kutokana na uwezo wa kila mchezaji, hivyo kilichobaki ni wote kupigania namba.

Hii pia ni kengele ya hatari inaanza kugonga kwa wachezaji wazawa, ambao baadhi yao wamebaki kucheza kwa mazoea, kwani makocha watakuwa wakichagua wachezaji wenye uwezo na wenye kujituma mazoezini tu bila kujali anatoka wapi.

Nasema ni kengele ya hatari kwenye vichwa vya wachezaji wa ndani, kwani kanuni hiyo imepitishwa wakati ambapo si Simba, Yanga wala Azam pekee ambazo zimesajili wachezaji wengi wa kigeni, bali hata zile timu ambazo hakuna yeyote aliyeamini kuwa watashusha 'maproo' kama Polisi Tanzania, Prisons, Mtibwa Sugar, Coastal Union, achilia mbali Namungo, Ihefu na Singida Big Stars.

Hii inaonyesha kuwa hakuna masihara, wachezaji wa Kitanzania wanatakiwa sasa kuvuta soksi ili kuwanyang'anya namba wageni kwa uwezo wao uwanjani.

Kwa hiyo wanatakiwa kujituma mazoezini, kuwa na nidhamu ndani na nje ya uwanja na kupunguza anasa ambazo huwafanya leo wacheze vizuri, lakini kesho wakionekana si kama siyo yule wa jana.

TANGAZO

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA KILIMO
# MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

## ORODHA YA MAWAKALA WALIOSAJILIWA KUSAMBAZA MBOLEA YA RUZUKU KWA MWAKA 2022/2023

### AWAMU YA KWANZA

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali inatarajia kutoa ruzuku ya mbolea kwa lengo la kuwawezesha wakulima nchini kununua mbolea kwa bei himilivu. TFRA ikiwa Mdhibiti wa mbolea inawasilisha awamu ya kwanza ya orodha ya mawakala ambao watauza na kusambaza mbolea za ruzuku kwa wakulima hapa nchini.

**ORODHA YA MAWAKALA WALIOSAJILIWA KUUZA NA KUSAMBAZA MBOLEA ZA RUZUKU**

| Na. | Jina la wakala | Na. ya wakala | Wilaya | Mkoa | Jina la Muagizaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | FEDELINA YAHAYA MAHENGE | TFRA-07-024 | MUFINDI DISTRICT COUNCIL | IRINGA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 2 | SEBASTIAN MUSA MUGANYA | TFRA-07-025 | KASULU DISTRICT COUNCIL | KIGOMA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 3 | HARSHO TRADING COMPANY LIMITED | TFRA-07-001 | MOSHI CBD DISTRICT COUNCIL | KILIMANJARO | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 4 | RAFIKI KILIMO LIMITED | TFRA-07-003 | MOSHI CBD DISTRICT COUNCIL | KILIMANJARO | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 5 | SUNGURA GENERAL SUPPLIES CO. LTD | TFRA-07-004 | HAI DISTRICT COUNCIL | KILIMANJARO | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 6 | COSTER SALEHE KASEBWA | TFRA-07-002 | MBEYA CBD DISTRICT COUNCIL | MBEYA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 7 | KERRY MBALALILA | TFRA-07-005 | MBEYA CBD DISTRICT COUNCIL | MBEYA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 8 | SUFIAN ISRAEL MAHENGE | TFRA-07-007 | MBEYA CBD DISTRICT COUNCIL | MBEYA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 9 | WILLIAM MEMBA MWANGOMILE | TFRA-07-006 | MBEYA DISTRICT COUNCIL | MBEYA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 10 | KIJANI KIZURI | TFRA-07-023 | MOROGORO CBD DISTRICT COUNCIL | MOROGORO | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 11 | KILOSA AGROVET SUPPLIES | TFRA-07-022 | KILOSA DISTRICT COUNCIL | MOROGORO | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 12 | MHEMA AGROCHEMICALS & GENERAL SUPPLIES | TFRA-07-012 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 13 | MTEWELE GENERAL TRADERS | TFRA-07-013 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 14 | DOMISIANA AGUSTINO KAPINGA | TFRA-07-016 | MBINGA DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 15 | JACKSON JOSEPH MAPUNDA | TFRA-07-017 | SONGEA DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 16 | JOHN SIXMUND MKINGA | TFRA-07-015 | SONGEA DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 17 | KASTORY ERICK TWEVE | TFRA-07-018 | SONGEA CBD DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 18 | LAMECK DAUD NGONACHE | TFRA-07-021 | SONGEA DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 19 | LESSA S. MBILINYI | TFRA-07-020 | SONGEA DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 20 | MICHAEL ALPHONCE MDETE | TFRA-07-014 | TUNDURU DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 21 | SHAMA BARNABAS MKUWA | TFRA-07-019 | SONGEA DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 22 | NDIYOKO FARM SUPPLIES | TFRA-07-026 | SHINYANGA CBD DISTRICT COUNCIL | SHINYANGA | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 23 | EMMANUEL MLOTWA NZYUNJE | TFRA-07-011 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 24 | ISSAH SAIMON SANGA | TFRA-07-008 | MOMBA DISTRICT COUNCIL | SONGWE | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 25 | MARTIN B. MTAFYA | TFRA-07-009 | ILEJE DISTRICT COUNCIL | SONGWE | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 26 | WILLIAM THOM LEMA | TFRA-07-010 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | DRTC TRADING COMPANY LTD |
| 27 | ETG - B 2763768 - ARUSHA | TFRA-06-002 | ARUSHA DISTRICT COUNCIL | ARUSHA | ETG INPUTS LIMITED |
| 28 | ETG - B 3898340 - KARATU | TFRA-06-025 | KARATU DISTRICT COUNCIL | ARUSHA | ETG INPUTS LIMITED |
| 29 | ETG - B 20000025657 - DAR ES SALAAM | TFRA-06-001 | TEMEKE DISTRICT COUNCIL | DAR ES SALAAM | ETG INPUTS LIMITED |
| 30 | ETG - B 4297504 - IRINGA | TFRA-06-004 | IRINGA DISTRICT COUNCIL | IRINGA | ETG INPUTS LIMITED |
| 31 | ETG - B 3747256 - MPANDA | TFRA-06-022 | MPANDA DISTRICT COUNCIL | KATAVI | ETG INPUTS LIMITED |
| 32 | ETG - B 03462123 - KIGOMA | TFRA-06-006 | KIGOMA CBD DISTRICT COUNCIL | KIGOMA | ETG INPUTS LIMITED |
| 33 | ETG - B 3594899 - KASULU | TFRA-06-007 | KASULU DISTRICT COUNCIL | KIGOMA | ETG INPUTS LIMITED |
| 34 | ETG - B 3970584 - MOSHI | TFRA-06-015 | MOSHI CBD DISTRICT COUNCIL | KILIMANJARO | ETG INPUTS LIMITED |
| 35 | ETG - B 3673848 - BABATI | TFRA-06-003 | BABATI CBD DISTRICT COUNCIL | MANYARA | ETG INPUTS LIMITED |
| 36 | ETG - B 3696143 - MBALIZI | TFRA-06-010 | MBEYA CBD DISTRICT COUNCIL | MBEYA | ETG INPUTS LIMITED |
| 37 | ETG - B 4098201 - TUKUYU | TFRA-06-013 | RUNGWE DISTRICT COUNCIL | MBEYA | ETG INPUTS LIMITED |
| 38 | ETG - B 4102665 - MBEYA | TFRA-06-009 | MBEYA CBD DISTRICT COUNCIL | MBEYA | ETG INPUTS LIMITED |
| 39 | ETG - B 3787975 - MOROGORO | TFRA-06-014 | MOROGORO CBD DISTRICT COUNCIL | MOROGORO | ETG INPUTS LIMITED |
| 40 | ETG - B 3915978 - MTWARA | TFRA-06-021 | MTWARA DISTRICT COUNCIL | MTWARA | ETG INPUTS LIMITED |
| 41 | ETG - B 3991364 - MASASI | TFRA-06-023 | MASASI DISTRICT COUNCIL | MTWARA | ETG INPUTS LIMITED |
| 42 | ETG - B 3870435 - MWANZA | TFRA-06-016 | NYAMAGANA DISTRICT COUNCIL | MWANZA | ETG INPUTS LIMITED |
| 43 | ETG - B 3924003 - NJOMBE | TFRA-06-017 | NJOMBE CBD DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ETG INPUTS LIMITED |
| 44 | ETG - B 41612775 - MAKAMBAKO | TFRA-06-008 | NJOMBE CBD DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ETG INPUTS LIMITED |
| 45 | ETG - B 3686125 - SUMBAWANGA | TFRA-06-019 | SUMBAWANGA DISTRICT COUNCIL | RUKWA | ETG INPUTS LIMITED |
| 46 | ETG - B 3831941 - SONGEA | TFRA-06-018 | SONGEA CBD DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | ETG INPUTS LIMITED |
| 47 | ETG - B 3812870 - KAHAMA | TFRA-06-005 | KAHAMA DISTRICT COUNCIL | SHINYANGA | ETG INPUTS LIMITED |

216989202

Inaendeleauk 8

# TANGAZO

Inatoka uk 7

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 48 | ETG - B 3913417 - TUNDUMA | TFRA-06-024 | MOMBA DISTRICT COUNCIL | SONGWE | ETG INPUTS LIMITED |
| 49 | ETG - B 3915978 - MBOZI | TFRA-06-011 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | ETG INPUTS LIMITED |
| 50 | ETG - B 3915979 - MLOWO | TFRA-06-012 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | ETG INPUTS LIMITED |
| 51 | ETG - B 3905946 - TABORA | TFRA-06-020 | TABORA CBD DISTRICT COUNCIL | TABORA | ETG INPUTS LIMITED |
| 52 | METL - ARUSHA | TFRA-05-003 | ARUSHA DISTRICT COUNCIL | ARUSHA | MOHAMMED ENTERPRISES TANZANIA LIMITED |
| 53 | GALU AGRO GENERAL SUPPLIES LTD. | TFRA-05-007 | KINONDONI DISTRICT COUNCIL | DAR ES SALAAM | MOHAMMED ENTERPRISES TANZANIA LIMITED |
| 54 | METL - ILALA | TFRA-05-001 | ILALA DISTRICT COUNCIL | DAR ES SALAAM | MOHAMMED ENTERPRISES TANZANIA LIMITED |
| 55 | METL - MBEYA | TFRA-05-005 | MBEYA DISTRICT COUNCIL | MBEYA | MOHAMMED ENTERPRISES TANZANIA LIMITED |
| 56 | FALELI ENTERPRISES COMPANY LTD. | TFRA-05-006 | ILEMELA DISTRICT COUNCIL | MWANZA | MOHAMMED ENTERPRISES TANZANIA LIMITED |
| 57 | MWAKILAVILE INVENSTMENT LIMITED | TFRA-05-008 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | MOHAMMED ENTERPRISES TANZANIA LIMITED |
| 58 | METL - SONGEA | TFRA-05-002 | SONGEA CBD DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | MOHAMMED ENTERPRISES TANZANIA LIMITED |
| 59 | METL - KAHAMA | TFRA-05-004 | KAHAMA DISTRICT COUNCIL | SHINYANGA | MOHAMMED ENTERPRISES TANZANIA LIMITED |
| 60 | FRANK BERNARD SANGA | TFRA-15-021 | IRINGA DISTRICT COUNCIL | IRINGA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 61 | OCP TANZANIA WAREHOUSE -IRINGA | TFRA-15-036 | IRINGA DISTRICT COUNCIL | IRINGA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 62 | MATAMBA 11 CO.LTD | TFRA-15-018 | MPANDA DISTRICT COUNCIL | KATAVI | OCP TANZANIA LIMITED |
| 63 | OCP TANZANIA WAREHOUSE -MPANDA | TFRA-15-028 | MPANDA DISTRICT COUNCIL | KATAVI | OCP TANZANIA LIMITED |
| 64 | SEBASTIAN MUSSA MUGANYA | TFRA-15-025 | KASULU DISTRICT COUNCIL | KIGOMA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 65 | OCP TANZANIA WAREHOUSE-KILIMANJARO | TFRA-15-027 | MOSHI CBD DISTRICT COUNCIL | KILIMANJARO | OCP TANZANIA LIMITED |
| 66 | MPANDILAH GENERAL SUPPLIES CO LIMITED | TFRA-15-039 | RUNGWE DISTRICT COUNCIL | MBEYA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 67 | MUSSA EPHRAIM MWAFONGO | TFRA-15-014 | RUNGWE DISTRICT COUNCIL | MBEYA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 68 | MWANJELWA AGROVET | TFRA-15-015 | MBEYA CBD DISTRICT COUNCIL | MBEYA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 69 | OCP TANZANIA WAREHOUSE -MBALIZI | TFRA-15-034 | MBEYA DISTRICT COUNCIL | MBEYA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 70 | OCP TANZANIA WAREHOUSE -RUNGWE | TFRA-15-031 | RUNGWE DISTRICT COUNCIL | MBEYA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 71 | OCP TANZANIA WAREHOUSE- MBEYA TOWN | TFRA-15-035 | MBEYA DISTRICT COUNCIL | MBEYA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 72 | OCP TANZANIA WAREHOUSE-UYOLE | TFRA-15-038 | MBEYA DISTRICT COUNCIL | MBEYA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 73 | SULI MALIKA MWANGWALE | TFRA-15-016 | MBEYA DISTRICT COUNCIL | MBEYA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 74 | AYUBU TRADING COMPANY | TFRA-15-022 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 75 | MHEMA AGROCHEMICALS & GENERAL SUPPLIES | TFRA-15-019 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 76 | MTEWELE GENERAL TRADERS & INSURANCE AGENT | TFRA-15-020 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 77 | OCP TANZANIA WAREHOUSE- MAKAMBAKO | TFRA-15-030 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 78 | OCP TANZANIA WAREHOUSE-NJOMBE | TFRA-15-029 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 79 | IKUWO GENERAL SUPPLIES | TFRA-15-017 | SUMBAWANGA DISTRICT COUNCIL | RUKWA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 80 | OCP TANZANIA WAREHOUSE-SUMBAWANGA | TFRA-15-026 | SUMBAWANGA CBD DISTRICT COUNCIL | RUKWA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 81 | BOFRA MICROFINANCE CO. LTD | TFRA-15-023 | SONGEA DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 82 | OCP TANZANIA WAREHOUSE-SONGEA | TFRA-15-033 | SONGEA DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 83 | SAMBALA FARMER'S CHOICE | TFRA-15-024 | SONGEA DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | OCP TANZANIA LIMITED |
| 84 | CHERNES MBUGHI | TFRA-15-001 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 85 | DAVID B. MAHENGE | TFRA-15-004 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 86 | EDISON A. MTAFYA | TFRA-15-007 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 87 | EMMANUEL ZYUNJE | TFRA-15-005 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 88 | GIDIONI KAYANGE | TFRA-15-009 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 89 | JONATHAMU P.KALINGA | TFRA-15-008 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 90 | MBUGHULA CO.LTD | TFRA-15-010 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 91 | MENART MZUMBWE | TFRA-15-002 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 92 | MENSON KIBONA | TFRA-15-003 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 93 | MSHANX AGROVET | TFRA-15-013 | MOMBA DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 94 | OCP TANZANIA WAREHOUSE-SONGWE | TFRA-15-032 | SONGWE DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 95 | OCP TANZANIA WAREHOUSE-TUNDUMA | TFRA-15-037 | MOMBA DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 96 | RICHARD A. KALONGE | TFRA-15-011 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 97 | UNYIHA ASSOCIATES | TFRA-15-012 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 98 | VICENT MWASHAMBWA | TFRA-15-006 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | OCP TANZANIA LIMITED |
| 99 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B03467187 - MUFINDI | TFRA-03-006 | MUFINDI DISTRICT COUNCIL | IRINGA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 100 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3696045 - MBEYA | TFRA-03-041 | MBEYA CBD DISTRICT COUNCIL | MBEYA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 101 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3871687 - IRINGA DC | TFRA-03-001 | IRINGA CBD DISTRICT COUNCIL | IRINGA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 102 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3871686 - IRINGA DC | TFRA-03-002 | IRINGA CBD DISTRICT COUNCIL | IRINGA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 103 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3871688 - IRINGA DC | TFRA-03-003 | IRINGA CBD DISTRICT COUNCIL | IRINGA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 104 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3871687 - IRINGA DC | TFRA-03-004 | IRINGA CBD DISTRICT COUNCIL | IRINGA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 105 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3873190 - MAFINGA DC | TFRA-03-005 | MAFINGA DC* | IRINGA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 106 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3877799 - KILOLO | TFRA-03-007 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |

Inaendeleo uk 9

# TANGAZO

Inatoka uk 8

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 107 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3877800 - KILOLO | TFRA-03-008 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 108 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3875897 - MUFINDI | TFRA-03-009 | MUFINDI DISTRICT COUNCIL | IRINGA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 109 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3877851 - KILOLO | TFRA-03-010 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 110 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B4099204 - CHUNYA | TFRA-03-011 | CHUNYA DISTRICT COUNCIL | MBEYA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 111 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B4099203 - CHUNYA | TFRA-03-012 | CHUNYA DISTRICT COUNCIL | MBEYA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 112 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B1317742 - ILEJE | TFRA-03-013 | ILEJE DISTRICT COUNCIL | SONGWE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 113 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B4101002 - MBEYA | TFRA-03-014 | MBEYA CBD DISTRICT COUNCIL | MBEYA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 114 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3916750 - MBOZI | TFRA-03-015 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 115 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3916751 - MBOZI | TFRA-03-016 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 116 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - N1316749 - MBOZI | TFRA-03-017 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 117 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B1316752 - MBOZI | TFRA-03-018 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 118 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3913875 - ILEJE | TFRA-03-019 | ILEJE DISTRICT COUNCIL | SONGWE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 119 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3696033 - MBEYA | TFRA-03-020 | MBEYA CBD DISTRICT COUNCIL | MBEYA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 120 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3695826 - MBEYA | TFRA-03-021 | MBEYA CBD DISTRICT COUNCIL | MBEYA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 121 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3698133 - CHUNYA | TFRA-03-022 | CHUNYA DISTRICT COUNCIL | MBEYA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 122 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3695825 - MBEYA | TFRA-03-023 | MBEYA CBD DISTRICT COUNCIL | MBEYA | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 123 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3632229 - MBOZI | TFRA-03-024 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 124 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3632228 - MBOZI | TFRA-03-025 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 125 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3923218 - WANGING'OMBE | TFRA-03-026 | WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 126 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3923221 - WANGING'OMBE | TFRA-03-027 | WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 127 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3923220 - WANGING'OMBE | TFRA-03-028 | WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 128 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3923217 - WANGING'OMBE | TFRA-03-029 | WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 129 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3923219 - WANGING'OMBE | TFRA-03-030 | WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 130 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3923222 - WANGING'OMBE | TFRA-03-031 | WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 131 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3923223 - WANGING'OMBE | TFRA-03-032 | WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 132 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3923224 - WANGING'OMBE | TFRA-03-033 | WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 133 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3925303 - NJOMBE TC | TFRA-03-034 | NJOMBE CBD DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 134 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3925302 - NJOMBE TC | TFRA-03-035 | NJOMBE CBD DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 135 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3925300 - NJOMBE TC | TFRA-03-036 | NJOMBE CBD DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 136 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3925301 - NJOMBE TC | TFRA-03-037 | NJOMBE CBD DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 137 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3924786 - NJOMBE RURAL | TFRA-03-038 | NJOMBE CBD DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 138 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3924787 - NJOMBE RURAL | TFRA-03-039 | NJOMBE CBD DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 139 | ONE ACRE TANZANIA LIMITED - B3925304 - NJOMBE TC | TFRA-03-040 | NJOMBE CBD DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | ONE ACRE TANZANIA LIMITED |
| 140 | ABISAI MEDRICK NGATA | TFRA-13-010 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 141 | ALLY RAMADHANI NGULUGULU | TFRA-13-007 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 142 | ATHUMANI HASHIM ABDALAH | TFRA-13-011 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 143 | DEO MAMBOLEO KAYUGWA | TFRA-13-006 | IRINGA DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 144 | DEOGRATUS JOHN SANGA | TFRA-13-016 | IRINGA CBD DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 145 | DORICE SAMWEL KITIME | TFRA-13-012 | IRINGA DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 146 | EDWARD ELEUTERI KAVIKULE | TFRA-13-008 | IRINGA DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 147 | FERDNANT MHEHE | TFRA-13-003 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 148 | HARD LAMECK NGWARE | TFRA-13-009 | IRINGA DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 149 | JOEL MSEWA | TFRA-13-004 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 150 | MBONEA FRANSIS SEGESELA | TFRA-13-013 | IRINGA DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 151 | NACOLI EBISON NGAIRO | TFRA-13-015 | IRINGA DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 152 | RAHABU JAMES N'GUMBI | TFRA-13-002 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 153 | THEO BATISTA MNGANDA | TFRA-13-014 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 154 | VITENDO NDANDANGO | TFRA-13-005 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 155 | ZABIBU MAGAVA | TFRA-13-001 | KILOLO DISTRICT COUNCIL | IRINGA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 156 | AYUB DANIEL MKEYA | TFRA-13-036 | WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 157 | BENEDICT ERENESIUS MASASI | TFRA-13-026 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 158 | FARAJA SAGO | TFRA-13-027 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |

Inaendeleo uk 10

# TANGAZO

Inatoka uk 9

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 159 | JANE WILBART ILOMO | TFRA-13-032 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 160 | JOHN KAROBA MAKONA | TFRA-13-030 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 161 | LINUS GASPER CHAMGENZI | TFRA-13-033 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 162 | LUKELO AGROCHEMICAL CENTER | TFRA-13-028 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 163 | MUSA ERENESIUS MASASI | TFRA-13-031 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 164 | NGAIRO AGROVET | TFRA-13-029 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 165 | NICOLINA ALOIS NDAVALA | TFRA-13-034 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 166 | RICHARD AMOS NYAGAWA | TFRA-13-037 | NJOMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 167 | SADICK SAMULI NZIKU | TFRA-13-035 | WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 168 | BROBY AGROVET | TFRA-13-022 | SUMBAWANGA DISTRICT COUNCIL | RUKWA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 169 | ETGE AGROVET | TFRA-13-024 | SUMBAWANGA DISTRICT COUNCIL | RUKWA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 170 | FREDY MWANYILA | TFRA-13-017 | KALAMBO DISTRICT COUNCIL | RUKWA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 171 | MWAKIBINGA AGROVET | TFRA-13-021 | SUMBAWANGA DISTRICT COUNCIL | RUKWA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 172 | PETER SEMUYEMBA | TFRA-13-019 | KALAMBO DISTRICT COUNCIL | RUKWA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 173 | SELEMAN AGROVET | TFRA-13-025 | SUMBAWANGA DISTRICT COUNCIL | RUKWA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 174 | SIMON SHAULI | TFRA-13-018 | SUMBAWANGA DISTRICT COUNCIL | RUKWA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 175 | SODOMA AGROVET | TFRA-13-020 | KALAMBO DISTRICT COUNCIL | RUKWA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 176 | TENGA NAMBA | TFRA-13-023 | KALAMBO DISTRICT COUNCIL | RUKWA | SKY MWAMOTO LIMITED |
| 177 | MBUYUNI AGROVET | TFRA-01-038 | KARATU DISTRICT COUNCIL | ARUSHA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 178 | TWINO ENTERPRISES LTD | TFRA-01-017 | ARUSHA CBD DISTRICT COUNCIL | ARUSHA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 179 | TATU KIMOLI PAULO / YOHANA AGR | TFRA-01-004 | GEITA DISTRICT COUNCIL | GEITA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 180 | ALPHA AGROVETS SUPPLIERS LTD | TFRA-01-002 | IRINGA CBD DISTRICT COUNCIL | IRINGA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 181 | FEDELINA YAHAYA MAHENGE | TFRA-01-027 | MUFINDI DISTRICT COUNCIL | IRINGA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 182 | MAFINGA FARMERS CENTRE | TFRA-01-010 | MUFINDI DISTRICT COUNCIL | IRINGA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 183 | MATAMBA II ENTERPRISES CO. LTD | TFRA-01-009 | MPANDA DISTRICT COUNCIL | KATAVI | YARA TANZANIA LIMITED |
| 184 | SEBASTIAN MUSSA MUGANYA | TFRA-01-019 | KASULU DISTRICT COUNCIL | KIGOMA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 185 | YOTHAM MBWILA TANDITSE | TFRA-01-020 | KASULU DISTRICT COUNCIL | KIGOMA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 186 | HAPCO AGRO BUSINESS | TFRA-01-015 | MOSHI CBD DISTRICT COUNCIL | KILIMANJARO | YARA TANZANIA LIMITED |
| 187 | NASA KILIMO ENTERPRISE | TFRA-01-040 | MOSHI CBD DISTRICT COUNCIL | KILIMANJARO | YARA TANZANIA LIMITED |
| 188 | SUNGURA GENERAL SUPPLIES | TFRA-01-016 | HAI DISTRICT COUNCIL | KILIMANJARO | YARA TANZANIA LIMITED |
| 189 | TEMBA AGROVET | TFRA-01-042 | ROMBO DISTRICT COUNCIL | KILIMANJARO | YARA TANZANIA LIMITED |
| 190 | TUKUTAANE AGROVERT | TFRA-01-041 | SAME DISTRICT COUNCIL | KILIMANJARO | YARA TANZANIA LIMITED |
| 191 | ABIHUDI MWATEBELA MWAMBEGELE | TFRA-01-030 | RUNGWE DISTRICT COUNCIL | MBEYA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 192 | ANTIOCH INVESTMENT | TFRA-01-005 | KYELA DISTRICT COUNCIL | MBEYA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 193 | EPHRAIM AMBONISYE MWAKILEMBE | TFRA-01-024 | MBARALI DISTRICT COUNCIL | MBEYA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 194 | HIGHLAND ESTATES LIMITED | TFRA-01-006 | MBARALI DISTRICT COUNCIL | MBEYA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 195 | OBO INVESTMENT LIMITED | TFRA-01-007 | MBEYA DISTRICT COUNCIL | MBEYA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 196 | PETRO EMILY FUNGO | TFRA-01-029 | RUNGWE DISTRICT COUNCIL | MBEYA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 197 | AGRINATURE COMPANY LTD | TFRA-01-008 | MOROGORO CBD DISTRICT COUNCIL | MOROGORO | YARA TANZANIA LIMITED |
| 198 | IPYANA EDWIN KAYUNI | TFRA-01-021 | KILOMBERO DISTRICT COUNCIL | MOROGORO | YARA TANZANIA LIMITED |
| 199 | PACHAMA TANZANIA LTD | TFRA-01-012 | NYAMAGANA DISTRICT COUNCIL | MWANZA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 200 | JAMES ISMAEL MNDELE | TFRA-01-022 | NJOMBE CBD DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | YARA TANZANIA LIMITED |
| 201 | MTEWELE GENERAL TRADERS | TFRA-01-011 | NJOMBE CBD DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | YARA TANZANIA LIMITED |
| 202 | ONES LUDZABIKO KATAWA | TFRA-01-037 | WANGING'OMBE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | YARA TANZANIA LIMITED |
| 203 | TULLY GWERINO MWASANGA | TFRA-01-023 | MAKETE DISTRICT COUNCIL | NJOMBE | YARA TANZANIA LIMITED |
| 204 | BEDA MAJALIWA SINKAMBA | TFRA-01-033 | SUMBAWANGA CBD DISTRICT COUNCIL | RUKWA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 205 | ESSAU SIMONY PELLA | TFRA-01-035 | TUNDURU DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 206 | TUMAINIEL JEFTA SANGA | TFRA-01-032 | SONGEA CBD DISTRICT COUNCIL | RUVUMA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 207 | NDIYOKO FARM SUPPLIES | TFRA-01-031 | SHINYANGA CBD DISTRICT COUNCIL | SHINYANGA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 208 | NG'WANAIBENGWE | TFRA-01-003 | KAHAMA DISTRICT COUNCIL | SHINYANGA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 209 | MLOBEZI MAFWELE | TFRA-01-018 | BUSEGA DISTRICT COUNCIL | SIMIYU | YARA TANZANIA LIMITED |
| 210 | SUZANA LAMECK SABUNI | TFRA-01-001 | BARIADI DISTRICT COUNCIL | SIMIYU | YARA TANZANIA LIMITED |
| 211 | CHARLES ABAS NDEMBWIKE | TFRA-01-034 | MOMBA DISTRICT COUNCIL | SONGWE | YARA TANZANIA LIMITED |
| 212 | UNDALI FARMERS CENTRE | TFRA-01-026 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | YARA TANZANIA LIMITED |
| 213 | VICENT SIMON MWASHAMBWA | TFRA-01-025 | MBOZI DISTRICT COUNCIL | SONGWE | YARA TANZANIA LIMITED |
| 214 | BRIDES AGROVERT/BRIAN VICTOR CHAMI | TFRA-01-013 | TABORA CBD DISTRICT COUNCIL | TABORA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 215 | GILIGWA MATHIAS GILIGWA | TFRA-01-036 | URAMBO DISTRICT COUNCIL | TABORA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 216 | JOHN STANLEY SONGO | TFRA-01-028 | NZEGA DISTRICT COUNCIL | TABORA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 217 | NGELELA AGROVET CO LTD | TFRA-01-014 | TABORA CBD DISTRICT COUNCIL | TABORA | YARA TANZANIA LIMITED |
| 218 | MCHINA AGROINPUTS | TFRA-01-039 | LUSHOTO DISTRICT COUNCIL | TANGA | YARA TANZANIA LIMITED |

**Dkt. Stephan E. Ngailo**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**12/08/2022**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

**Kwa taarifa zaidi:**

***Tembelea ofisi yetu iliyopo Kitalu Na. 15471, 1 Mtaa wa Kilimo, Jengo la Kilimo I, S. L. P. 46238, Dar es salaam, Tanzania au piga +255222861939.***

216989202

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 7 EPL WANAOLIPWA FEDHA NYINGI ZAIDI 2022-23 UK. 12-13




# 5-BORA YA UHAMISHO HURU MSIMU HUU

## ISIKUPITE

ACHANA na hat-trick, katika karne hii ya 21, Lionel Messi na Cristiano Ronaldo ndiyo wachezaji wanaongoza kwa kufunga mabao mawili katika mchezo mmoja ('braces') kwenye mashindano yote, wakifanya hivyo mara 205 kila mmoja, wakifuatiwa na Robert Lewandowski (135), Zlatan Ibrahimovic (98) na Karim Benzema (87).



**LONDON,** England

HUKU ulimwengu wa soka ukiingia kwenye mwanzo wa msimu wa 2022-23, dirisha la uhamisho wa majira ya joto limekuwa likiendelea kwa miezi michache iliyopita. Klabu zote Ulaya zinajaribu kuimarisha vikosi vyao kwa ajili ya mataji, kupanda daraja na kuepuka kushuka daraja, miongoni mwa malengo mengine mengi.

Majina makubwa ya kawaida kama Manchester City, Barcelona, Bayern Munich, Manchester United, na wengineo wamekuwa wakifanya kazi sokoni, wakitumia fedha nyingi kupata majina bora kwenye mchezo huo.

Baadhi ya uhamisho wenye thamani ya juu hadi sasa ni Erling Haaland, Aurelien Tchouameni, Darwin Nunez, Matthijs de Ligt, na Raheem Sterling.

Pamoja na matumizi yote hayo, kumekuwa na manunuzi ya kijanja ya baadhi ya timu ambayo yamefanikiwa kusajili wachezaji wenye ubora kwa uhamisho wa bure. Hapa chini, tunaangalia uhamishaji wa bure wa wachezaji watano bora zaidi wa msimu huu wa majira ya joto, twende sasa...

### #1. Antonio Rudiger (Real Madrid)

Real Madrid walimaliza msimu uliopita kwa kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na lile la LaLiga. Hata hivyo, hawatazamii kupumzika kwa kuwa wanalenga kupata mataji zaidi.

'The Blancos' hao wamekuwa wakifanya kazi katika soko la usajili, na kufanikiwa kumsajili nyota wa Ufaransa, Tchouameni.

Hata hivyo, ni uhamisho wa bila malipo wa Antonio Rudiger kutoka Chelsea ambao unaweza kuwa bora zaidi. Nyota huyo wa zamani wa Chelsea ni mchezaji mwenye uzoefu akiwa na zaidi ya mechi 200 akiwa na 'The Blues' na 50 akiwa Ujerumani.

Mjerumani huyo ni mkabaji mgumu na mwepesi wa mawazo ya kushinda, anajulikana kusaidia kwa juhudi kubwa langoni. Kuongezwa kwake kwenye safu dhabiti ya nyuma ya kocha, Carlo Ancelotti, kutakifanya kikosi hicho kuwa bora zaidi kwenye ulinzi akishirikiana na David Alaba.

### #2. Franck Kessie (Barcelona)

Barcelona wamekuwa na shughuli nyingi msimu huu na idadi kubwa ya uhamisho wa hali ya juu. Majina kama vile Robert Lewandowski, Jules Kounde, Andreas Christensen na Raphinha, wote wamehamia Camp Nou kwa fedha nyingi.

Usajili wa Franck Kessie unaoonekana kama dili kubwa. Miongoni mwa nyota wanaochipukia katika safu ya kiungo barani Ulaya, raia huyo wa Ivory Coast alikuwa sehemu muhimu ya AC Milan kushinda taji la Serie A msimu uliopita. Kiungo mkabaji, Kessie anafahamika kulinda safu yake ya ulinzi na kuufanya mpira kwenda mbele.

Katika misimu miwili iliyopita, alifanikiwa kupata idadi nzuri ya mabao kutoka katikati na kufikisha jumla ya mabao 21. Anaweza kuongeza nguvu ya mabao ya ziada kwenye safu ya kiungo ya Barcelona, jambo ambalo huenda walilikosa misimu iliyopita.

Akiwa na umri wa miaka 25 tu, anaweza kuwa suluhu la muda mrefu la kiungo walilokuwa wanalihitaji 'Blaugrana' hao endapo Frenkie de Jong ataondoka.

### #3. Paulo Dybala (AS Roma)

Paulo Dybala aliwahi kuonekana kama mmoja wa vipaji angavu zaidi pale Juventus. Alifanikiwa kuanza kwa kasi na alikuwa akifunga mabao kwa kufurahisha na kuiongoza Juventus kutwaa mataji mengi ya Serie A.

Lakini, kazi yake haijabadilika kama vile mtu yeyote angetarajia. Bila kujali hilo, ana namba za ajabu kwa 'Kibibi Kizee cha Turin', akifunga mabao 115 katika michezo 293.

Jose Mourinho ameweza kumpata Dybala pale AS Roma na wanatumaini kwamba La Joya wanaweza kurejesha kiwango chao cha zamani kwa timu hiyo msimu huu.

### #4. Christian Eriksen (Manchester United)

Kuna hadithi chache za kutia moyo kuliko ile ya Christian Eriksen katika soka. Mchezaji huyo wa Denmark alipata mshtuko wa moyo wakati wa michuano ya Euro 2020, lakini amepambana kurejea mchezoni baada ya kusajiliwa na Brentford, Januari mwaka huu.

Sasa, mchezaji huyo wa zamani wa Tottenham Hotspurs anavaa nyekundu ya Manchester United. Ataendelea na safari yake ya Ligi Kuu. Amecheza zaidi ya michezo 200 kwa Spurs na Brentford na kuchangia zaidi ya mabao 100.

Kiungo wa darasa, Eriksen anaweza kutoa mwelekeo mpya kwa safu ya kati ya United ambayo mara nyingi imekuwa ikimtegemea Bruno Fernandes. Kwa hakika itampa kocha mpya Eric ten Hag chaguo jingine iwapo ataamua kumzungusha Fernandes au kuwatumia tu wachezaji wote wawili.

### #5. Paul Pogba (Juventus)

Juventus ndio vinara wa uhamisho wa bila malipo, kiasi kwamba walifanikiwa kumsajili Paul Pogba kwa mara ya pili akitokea Manchester United. Mfaransa huyo alitumia misimu sita ya kusumbua kule England.

Kulikuwa na picha chache za vipaji ambavyo viliifanya United kulipa ada ya rekodi kwa mhitimu wao wa akademi, lakini mambo yalikuwa tofauti na mashabiki walivyotarajiwa.


Hatimaye, baada ya kumaliza mkataba wake, mshindi huyo wa Kombe la Dunia amerejea pale alipoibuka kidedea. Kabla ya kuhamia United, Pogba lilikuwa jina la ushawishi kwa Juventus kwa mabao yake na uwezo wake wa kupiga pasi.

Lakini litakuwa jambo la kufurahisha kuona ikiwa kweli anaweza kurejea kwenye kiwango chake.

Kwa sasa, Pogba yuko nje ya uwanja kutokana na jeraha la muda mrefu ambalo linaweza kumuweka nje ya uwanja kwa takribani miezi miwili kwani ameamua kutokwenda kufanyiwa upasuaji kwa nia ya kucheza Kombe la Dunia baadaye mwaka huu.

Time

# WACHEZAJI 7 EPL WANAOLIPWA FEDHA NYINGI ZAIDI 2022-23



RONALDO

**LONDON,** England

LIGI Kuu ya soka England (EPL), ndio tajiri zaidi katika sayari hii. Kwa kuwa ligi inayoonyeshwa zaidi kwenye televisheni, timu hupata kiasi kikubwa cha fedha kupitia mikataba ya haki za matangazo ya TV ya ndani na nje ya nchi.

**Kuongeza ufadhili na uidhinishaji mbalimbali kwa mchanganyiko, hata timu za katikati zinaanza kuonekana kuwa tajiri kuliko klabu za hali ya juu katika ligi zingine za Ulaya.**

Kwa kuwa na fedha nyingi zinazunguka, haishangazi kwa klabu kuwatumia wachezaji wanaowataka. Wanatoa mishahara mikubwa na marupurupu mengine mengi kwa wachezaji, na kuwafanya kuwa baadhi ya wanamichezo matajiri zaidi duniani.

Makala haya inawaangalia wachezaji saba wa Ligi Kuu England ambao huchukuwa fedha nyingi zaidi kuliko wengi wanavyoweza kufikiria.

Hawa ndio wachezaji saba wanaolipwa fedha nyingi zaidi katika Ligi Kuu England kwa msimu wa huu 2022-23...

### #7. Raphael Varane (Manchester United) – Pauni mil. 17,680,000 kwa mwaka

Akiwa ameshinda kila kitu akiwa na Real Madrid, Raphael Varane alijiunga na Manchester United msimu uliopita wa majira ya joto.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018, akiwa na Ufaransa, alitia saini mkataba wa miaka minne wenye thamani ya pauni milioni 17,680,000 kwa mwaka na kumfanya kuwa beki anayelipwa fedha nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu England.

Akiwa mbali na Madrid kwa mara ya kwanza baada ya muongo mmoja, Varane hakuwa na msimu mzuri pale Man United msimu uliopita.

Si tu kwamba alijitahidi kutafuta kiwango chake, lakini alikuwa na majeraha ya mara kwa mara. Varane alimaliza msimu wa kwanza akiwa na mechi 22 za Ligi Kuu, akifunga mara moja na kutoa asisti moja.

Man United watatumaini kuwa mchezaji wao huyo nyota atajiimarisha zaidi kwenye msingi wa safu yao ya ulinzi msimu huu mpya.

### #6. Jadon Sancho (Manchester United) – Pauni mil. 18,200,000 kwa mwaka

Jadon Sancho, ambaye alijiunga na Manchester United kutoka Borussia Dortmund msimu uliopita wa majira ya joto, kwa sasa anapokea pauni pauni milioni 18,200,000 kwa mwaka, na kumfanya kuwa mmoja wa vijana wanaolipwa fedha nyingi zaidi.

Raia huyo wa England ingawa alikuwa na kipaji cha hali ya juu, hakuwa na msimu mzuri kwenye msimu wake wa kwanza wa Ligi Kuu, akiandikisha mabao matatu pekee katika mechi 29.

Chini ya kocha mpya Erik ten Hag, Sancho anatarajiwa kuwa kwenye kiwango bora ili apate nafasi ya kucheza mara kwa mara.

### #5. Mohamed Salah (Liverpool) – Pauni milioni 18,200,000 kwa mwaka

Tangu ajiunge nayo akitokea AS Roma mwaka 2017, Mohamed Salah ameendelea kutengeneza urithi wa kuvutia akiwa na Liverpool na kwenye Ligi Kuu.

Mchezaji Bora wa Mwaka wa PFA ameshinda Kiatu cha Dhahabu mara tatu na kuwasaidia 'Wekundu' hao kutwaa taji la Ligi Kuu mara moja. Kwa kuzingatia ubora anaoleta kwenye timu, mshahara wake wa pauni milioni 18,200,000 kwa mwaka hauonekani kuwa sawa.

Salah, ambaye hivi majuzi alitia saini nyongeza ya miaka miwili na Liverpool, alimaliza kampeni ya 2021-22 akiwa si tu mfungaji bora (mabao 23) bali pia mtoa pasi za mabao 13.

Alikuwa mchezaji bora wa Wekundu hao (bao moja na asisti) katika ushindi wao wa Ngao ya Jamii ya FA (3-1) dhidi ya Manchester City, Julai 30, mwaka huu. Salah kwa mara nyingine anatarajiwa kucheza nafasi muhimu kwa Liverpool msimu huu.

### #4. David de Gea (Manchester United) – Pauni mil. 19,500,000 kwa mwaka

Akipokea kitita cha pauni milioni 19,500,000 kwa mwaka, nyota wa Manchester United, David de Gea ndiye mchezaji wa pili anayelipwa zaidi kikosini hapo.

Kipa huyo wa zamani wa Atletico Madrid ni mmoja wa viongozi wasiopingika katika timu hiyo, anasimama vema katika nafasi yake.

De Gea ana changamoto mpya mbele yake, sasa akiwa chini ya kocha Erik ten Hag, kocha ambaye anapenda timu yake kucheza kwa kuanzia nyuma.

Hata hivyo, kutokana na uzoefu na ubora wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ana nafasi ya kufanya vizuri zaidi.

### #3. Erling Haaland (Manchester City) – Pauni mil. 19,500,000 kwa mwaka

Manchester City ilishinda kwenye mbio dhidi ya timu nyingi za Ulaya na kuipata huduma ya Erling Haaland, Julai mwaka huu akitokea Borussia Dortmund.

City inamlipa Haaland mshahara wa pauni milioni 19,500,000 kwa mwaka.

Katika miaka mitano ijayo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, atakuwa amepata karibu pauni milioni 100,000,000 za mshahara, na bado atakuwa na fursa ya kufanya uhamisho mwingine wa fedha nyingi.

Haaland, ambaye anasifiwa kuwa mmoja wa washambuliaji bora katika biashara, amekuja Ligi Kuu akiwa na sifa kubwa.

### #2. Kevin De Bruyne (Manchester City) – Pauni mil. 20,800,000 kwa mwaka

Mchezaji bora wa Manchester City, Kevin De Bruyne anachukuwa pauni milioni 20,800,000 kwa mwaka, na kumfanya kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi hapo kwenye Uwanja wa Etihad.

Ingawa jumla ni ya juu sana, Mbelgiji huyo amefanya haki yake anayostahili. Zaidi ya miaka saba iliyopita, amejidhihirisha kama moyo wa timu, mara kwa mara akijikuta akivuta kamba kutoka katikati ya uwanja.

Mbali na kutoa pasi za ulinzi, kiungo huyo mshambuliaji pia anafunga mabao mazuri, huku sifa zake zote zikionyeshwa msimu wa 2021-22.

De Bruyne alifunga mabao 15 na kutoa asisti nane katika mechi 30 za Ligi Kuu msimu uliopita, akiibuka mfungaji bora wa timu hiyo.

Mchango wake wa mabao si tu uliisaidia Man City kutwaa taji lao la pili mfululizo la ligi.

### #1. Cristiano Ronaldo (Manchester United) – Pauni mil. 26,800,000 kwa mwaka

Mshindi mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or, Cristiano Ronaldo amekuwa akihaha kutaka kuhama kwenye Ligi Kuu England msimu huu wa 2022-23, kwani inadaiwa (kupitia Mirror) anataka kuhamia klabu inayocheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, ikiwa ataongeza muda wa kukaa Man United, ataishia kutwaa kitita cha pauni milioni 26,800,000, na kumfanya kuwa mwanamichezo anayelipwa zaidi.

Ronaldo na Harry Maguire ndio wanasoka wawili wanaokashifiwa zaidi kwenye Twitter katika klabu hiyo ya Man United.

Ronaldo alijiunga tena na United kutoka Juventus msimu uliopita wa majira ya joto na kuibuka mfungaji bora wa tatu kwenye Ligi Kuu msimu wa 2021-22, akifunga mabao 18 katika mechi 30.

Kocha mpya wa Man United, Erik ten Hag, bila shaka anaweza kutumia mabao yake, ndiyo maana wamekuwa wakisita kufanya mazungumzo ya kumwondoa.


Huku kampeni mpya ya Ligi Kuu ikiwa imeanza, Ronaldo anaonekana kuwa na uwezekano mkubwa wa kucheza angalau mechi chache kwenye msimu ujao.

## Nukuu

"Kipindi cha kwanza tulicheza vizuri, lakini kipindi cha pili kulikuwa na mabadiliko ya wachezaji wawili kwa Yanga na hatukuonyesha kuzingatia zaidi na mabeki wetu walifanya makosa, hivyo Yanga kufunga mabao mawili na kushinda mchezo, hongera kwao," **Kocha Mkuu wa Simba, Zoran Maki baada ya kupoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Yanga kwenye Ngao ya Jamii juzi.**



"Ni ujinga, jinsi tulivyocheza leo (juzi), lazima ucheze moja kwa moja zaidi. Unaweza kuwa na mpango, lakini tunaweka mpango kwenye pipa," **Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag baada ya timu yake kuchezea mabao 4-0 dhidi ya Brentford, Jumamosi.**



"Kipindi cha kwanza tuliona mapungufu, hivyo cha pili tukafanya mabadiliko kwanza kwa kumrudisha Azizi Ki katika nafasi yake anayocheza, kisha tukamwingiza Moloko [Jesus] ili kutuongezea kasi na Morrison [Bernard] kwa ajli ya kutusaidia kwa ubunifu wake, hivyo mabeki wao wakashindwa kupanda kwa kuogopa kasi yetu, kwa dakika zote 90 tulistahili ushindi," **Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Simba kwenye Ngao ya Jamii juzi.**





Fiston Mayele (wa pili kushoto), akishangilia sambamba na wachezaji wenzake wa Yanga baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Simba kwenye mechi ya Ngao ya Jamii iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA ILIPOFANIKIWA NA SIMBA KUTELEZA

**Na Adam Fungamwango**

SIMBA imepoteza mechi dhidi ya Yanga kwa mara nyingine tena, baada ya kuchapwa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Jumamosi iliyopita.

**Yalikuwa ni mabao ya Fiston Mayele, huku lile la kufutia machozi la Simba likifungwa na Pape Sakho.**

Hii ni kwa mara nyingine tena baada ya kupata kipigo cha bao 1-0 Mei 28 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, likiwekwa wavuni na Feisal Salum 'Fei Toto.'

Pia ni mara ya pili kwa Simba kufungwa kwenye mechi ya Ngao ya Jamii kwani mwaka jana, Septemba 25, Yanga ilishinda bao 1-0 likiwekwa wavuni na Mayele. Kwa miaka ya karibuni imeonekana Simba inahenyeka mbele ya Yanga, hata kama ikiwa na kikosi kizuri.

Pia, Yanga imeonekana kuwa na dawa ya kuitungua Simba kwa sasa, kwani tangu ikiwa na kikosi ambacho si imara, mpaka sasa ambapo kwa misimu hii miwili imeimarika, imeendelea kuwa mwiba mkali kwa watani wao ya jadi.

Yafuatayo ni mambo yaliyojitokeza kwenye mechi hiyo ambayo sasa imeashiria kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara itakayoanza leo.

**#1. Wageni wametetema na kunyunyiza**

Mabao yote matatu kwenye mechi hiyo, yamefungwa na wachezaji wa kimataifa wanaocheza soka la kulipwa nchini Tanzania. Ni tofauti na mechi ya mwisho zilipokutana ambapo Mbongo, Fei Toto ndiye aliyeibuka shujaa.

Straika hatari kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Mayele ndiye aliyefunga na kuendeleza staili yake ya kutetema, huku raia wa Senegal, Pape Sakho ambaye naye ana staili yake maarufu ya kunyunyiza akicheka na nyavu pia.

Wageni hawa wanaingia kwenye vitabu vya kumbukumbu vya wachezaji waliowahi kufunga mabao kwenye mechi za 'dabi'.

**#2. Mabao yote yamefungwa Kusini**

Pia mabao yote matatu kwenye mechi ya Jumamosi yalifungwa kwenye lango moja la kusini mwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Pape alifunga bao kipindi cha kwanza na hadi mapumziko, Simba ilikuwa ikiongoza kwa 1-0, huku kipindi cha pili Yanga nayo ilianza kupeleka mashambulizi yake upande wa kusini na kufanikiwa kufunga mabao yote mawili upande huo.

**#3. Simba inateseka na kiungo mkabaji**

Moja kati ya udhaifu wa Simba ambao utaendelea kuwatafuna kwa sababu ni kama vile wamelifumbia macho ni kiungo mkabaji. Watasajili kote, lakini sehemu hiyo huwa haichukuliwi kwa uzito stahiki na kama lisipoangalia litawatesa kwenye Ligi ya Mabingwa pia.

Ilitegemewa msimu huu itakuwa makini na hilo, lakini bado imeendelea kuwatumia kina Jonas Mkude na Mzamiru Yassin ambao ukweli mchungu ni kwamba wanachezea uzoefu tu na si kwa viwango vinavyotakiwa.

Kipindi cha kwanza, ilibebwa mno na Sadio Kanoute ambaye kwa kiasi kikubwa ndiye aliyekuwa akikata mawasiliano wa viungo wa Yanga bila usaidizi wowote wa maana kiasi cha kupata kadi ya njano.

Nadhani Kocha Mkuu wa Simba, Zoran Maki alimtoa kwa sababu ya kuhofia kadi nyekundu, baada ya hapo mambo yakaharibika kabisa.

**#4. Kocha Nabi aliligundua hilo**

Inawezekana kabisa Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi ameshawasoma Simba na kugundua kuwa wana matatizo kwenye kiungo mkabaji wa maana tangu walivyoondoka kina Gerson Fraga, James Kotei, na Thadeo Lwanga wakati yupo kwenye kiwango chake, ndiyo maana amekuwa akiisumbua kwa miaka yote miwili.

Ndiyo maana alimhamisha Stephane Aziz Ki pembeni na kumwingiza ndani kucheza kwenye 'shimo', akawa na kazi ya kuchukua mipira na kuanza kutembea kati akiwa hakabwi kiasi cha kuwasumbua mno mabeki wa Simba waliokosa usaidizi madhubuti wa kulindwa na viungo wakabaji, hali iliyowafanya waanze kukatika.

Kuna wakati Mohamed Ouattara akatoka na kusogea mbele kidogo ili acheze kama namba sita, baada ya kuona hakuna msaada wowote, akimuacha Henock Inonga peke yake nyuma.

**#5. Yanga ilitawala kina Chama walipotoka**

Pamoja na udhaifu wa kiungo cha ukabaji Simba, Clatous Chama, na Denis Kibu walipokuwa uwanjani, waliwalazimisha mabeki wa Yanga na viungo wao wasipande, na hii iliwapa kina Mkude unafuu, lakini walipotoka viungo wa timu hiyo, Aboubakar Salum 'Sure Boy', Yannick Bangala, Khalid Aucho na Fei Toto ambao kwa kiasi kikubwa waliwalinda mabeki wao wasifikiwe kirahisi, walianza kupanda na kusababisha madhara makubwa kwenye safu ya kiungo, na mabeki wa kati na pembeni wa Simba.

**JE, WAJUA?**



KATIKA karne hii ya 21 kwenye Ligi Kuu England, Cesc Fabregas bado ndiye mchezaji anayeshikilia rekodi ya kutoa pasi za mwisho nyingi ('assists') akifanya hivyo mara 118, huku akifuatiwa na Wayne Rooney (114), Ryan Giggs (110), David Silva (106) na Frank Lampard (100).





# Waelezwa umuhimu kuongeza thamani ya mazao

**Magdalena Jackson (SJMC) na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKULIMA wametakiwa kuongeza thamani ya mazao yao ili kukuza kipato cha biashara wanazozifanya na kuwainua kiuchumi.

Ofisa Mitihani na Udahili wa Chuo cha Mipango, Maendeleo Vijijini, Lightness Mlay, alitoa kauli hiyo hivi karibuni jijini hapo alipokuwa akizungumza na Nipashe, kwenye maonesho ya wakulima.

Alisema kuwa wakulima wengi hawana uelewa juu ya kuongeza thamani katika mazao yao, chuo chicho kilianzisha miradi miwili kwenye mikoa ya Dodoma na Mwanza ambayo imetumika kuwaelimisha kilimo chenye tija na ubora.

"Sisi kama chuo tunamwelimisha mkulima wa mahindi kuwa hatakiwi kuuza mahindi peke yake, bali bidhaa zote zitokanazo na zao hilo kama vile mabua, magunzi, pumba, unga na mafuta, vivyo hivyo kwa wavuvi kupata samaki pamoja na mafuta," alisema.

Alisema kuwa kwa kituo cha Kanda ya Ziwa kwa Wilaya ya Bunda na Ukerewe, mradi umejikita kuwaelimisha wafugaji juu ya ufugaji wenye manufaa na umesaidia kuongeza thamani ya bidhaa zao kwa kuwajengea kiwanda cha barafu.

Aliomba serikali kuwawezesha wakulima na wafugaji kutatua kero zao kwa kutoa elimu zaidi ya kuongeza thamani za bidhaa zao pamoja na kuwasaidia kifedha ili shughuli zao ziwe na tija.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano wa Chuo hicho, Godrick Ngoli, alihamasisha wakulima na wafugaji kushiriki sensa na kutoa taarifa sahihi ili kusaidia katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo.

"Watu wakishiriki na kutoa taarifa sahihi itarahisisha utambuzi wa mahitaji ya makundi mbalimbali kama vile vijana, wazee, walemavu, wasomi, na wafanya biashara ili kusaidia nchi kupanga mipango kwa ajili ya wananchi," alisema.

Ngoli alisema kwa hivi sasa chuo kina miradi ambayo imeleta tija kwa wananchi na mabadiliko ya kiuchumi katika maeneo manne ambayo ni Chololo, Kikombo, Miganga na Idifu jijini Dodoma.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Cyprian Luhemeje, akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa Idara ya Habari Maelezo jijini Dodoma mwisho wa wiki alipoelezea mafanikio na mwelekeo wa mamlaka hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/20223. **PICHA: IBRAHIM JOSEP**

# Wakulima kujisajili kuingia mfumo kupata mbolea

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

WAKATI bei za ruzuku ya mbolea zikianza kutumika leo, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imewataka wakulima kuendelea kujisajili ili kuingia kwenye mfumo wa kupata mbolea hiyo.

Hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan alielekeza wakulima kununua mbolea kwa bei ya ruzuku kuanzia Agosti 15, mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephan Ngailo, katika taarifa yake aliyoitoa mwishoni mwa wiki, alisema wakulima wote wanapaswa kujisajili kwenye mfumo ili kusajiliwa na kuipata mbolea hiyo kwa urahisi zaidi.

Alisema bila kufanya hivyo itawawia vigumu kwa kuwa kila kitu kimepangwa kutekeleza kwa njia ya mifumo ili kuepuka udanganyifu kwenye utoaji mbolea.

Kadhalika, alisema serikali imetenga Sh. bilioni 150 kwa ajili ya kugharamia ruzuku ya mbolea ambayo itatolewa kwa wakulima wote nchini ili kupunguza makali kutokana na soko la mbolea kupanda duniani.

Naye Kaimu Meneja wa Uhusiano, Mawasiliano na Elimu kwa Umma, Matilda Kasanga, alisema mamlaka hiyo imekuwa ikitoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kupitia Maofisa Ugani walioko katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha kila mkulima anapata uelewa.

Kasanga alisema ejitokzaidi ya wakulima 1,000 kwa kipindi kifupi wameza kupata elimu ili kuingia kwenye mfumo huo.

Alihimiza wakulima kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kujisajili kwenye mfumo ili kupata mbolea hiyo.

Alisema TFRA itaendelea kutoa elimu kwa wakulima ili kuhakikisha kila mkulima anapata fursa ya upatikanaji wa mbolea ya ruzuku kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

Katika ruzuku hiyo, mbolea aina ya DAP kwa mfuko wa kilo 50 utakuwa Sh. 70,000 baada ya kutoa ruzuku ya serikali ya Sh. 61,676, aina ya UREA itakuwa Sh. 70,000 baada ya kutoa ruzuku ya Sh. 54,734.

Mbolea ya CAN itakuwa Sh. 60,000 baada ya kutoa ruzuku ya Sh. 48,156, aina ya SA itakuwa Sh. 50,000 baada ya kutoa ruzuku Sh. 32,852 na aina ya NPKs itakuwa Sh. 70,000 baada ya kutoa ruzuku Sh. 52,695.

# Vijana wapewa mbinu kusaidia kutatua kero

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imetoa wito kwa vijana kubuni mifumo ya kimkakati itakayosaidia kutatua kero mbalimbali zinazoikabili jamii.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alitoa rai hiyo jana alipotembelea Ofisi za Mamlaka ya Serikali Mtandao katika Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGovRIDC), kilichoko Ndaki ya Sayansi ya Kompyuta, Habari na Mawasiliano - Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

"Ninaitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), kutafuta rasilimali fedha na kuweka mpango wa kimkakati wa namna ya kuongeza idadi ya vijana wanaokuja kufanya mafunzo kwa vitendo katika masuala ya TEHAMA ili kuchochea utafiti na ubunifu," alisema.

Mhagama alisema kuwa ujenzi wa kituo cha utafiti utachochea ari ya vijana kujifunza kwa vitendo na kuchangia katika ustawi wa taifa kupitia tafiti zinazofanywa hasa katika utatuzi wa kero mbalimbali za jamii.

"Endapo utafiti na ubunifu utaimarika, serikali itakuwa na mifumo ya kimkakati na kutakuwa na suala la ukusanyaji wa mapato litakuwa rahisi, mazingira ya uwekezaji na biashara yataimarika, usimamizi wa fedha za umma na utakuwa umeboreshwa na kutakuwa na upatikanaji wa huduma bora kwa umma kwa wakati na kwa gharama nafuu," alisema.

Mhagama alisema utekelezaji wa mifumo hiyo iende sambamba na usimamizi wa sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo iliyowekwa ili kuhakikisha jitihada za utekelezaji wa Serikali Mtandao zinaonekana na kufikia lengo la kuwa na uchumi wa kidijitali. Naye Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais hiyo, Xavier Daudi, alipongeza eGA kwa jitihada za utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini, Alisema mamlaka kupitia wanafunzi hao imefanya kazi kubwa ya utafiti na ubunifu wa mifumo inayosaidia serikali na kukuza matumizi ya TEHAMA nchini.

"Nawapongeza mamlaka, kama serikali tunatambua mnachokifanya na tunawatia moyo kama nchi tumesogea mbele na tunahitaji kusonga mbele zaidi katika masuala ya TEHAMA," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu eGA, Benedict Ndomba, amesema suala la utafiti na ubunifu linasaidia kwa kiasi kikubwa kuendeleza jitihada za serikali mtandao.

Alisema mamlaka imeongeza idadi ya wanafunzi wa mazoezi waliopita katika kituo hicho kutoka idadi ya wanafunzi 33 katika awamu ya kwanza hadi kufikia 72 katika awamu ya pili. "Kwa sasa mamlaka imepanga kuongeza uwezo wa kituo ili kuchukua wanafunzi 300 hadi 500 kwa wakati mmoja ili kuchochea ubunifu na utafiti katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao," alisema. Alisema mamlaka hiyo ilianzisha kituo hicho mwaka 2019 kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa umma kupitia utafiti na kufanya ubunifu katika maeneo mbalimbali.



# Wadau waomba ushirikiano kudhibiti ukatili kijinsia

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WADAU wa Masuala ya Ukatili wa Kijinsia katika Mkoa wa Mbeya wameomba ushirikiano kuanzia ngazi ya familia ili kukabiliana na vitendo vya ukatili.

Akizungumza juzi na Nipashe Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Mbeya, Loveness Mtemi, alisema kuwa lengo la mpango huo ni kutokomeza vitendo hivyo ambavyo ni vya ubakaji, ulawiti na vipigo.

Alisema licha ya wanawake na watoto kuwa waathirika wa matukio hayo kuna tatizo la watu hao kutotoa taarifa wanapofanyiwa vitendo vya kikatili.

"Kuna tatizo kubwa la vitendo vya ukatili wa kingono kwa wanawake na watoto, mbaya zaidi hawatoi ushirikiano kwa Jeshi la Polisi wanawakumbatia watuhumiwa kutokana na mahusiano waliyonayo kwenye familia zao naomba tubadilike," alisema Mtemi.

Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Annagloria Gereta, alisema hospitali hiyo imekuwa ikipokea watoto wengi ambao wanafanyiwa vitendo vya kikatili.

Alisema miongoni mwa vitendo vinavyoripotiwa ni ulawiti kwa watoto wa kiume na wa kike na wanapohitaji ushirikiano kutoka kwa wazazi wanakosa.

Alisema licha ya hospitali hiyo kupokea watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili, alidai mpango mkakati huo waliokubaliana katika kikao hicho utaleta tija kwa kuwa wataendelea kutoa elimu kwa kuwashirikisha wazazi na walezi.

Gereta aliongeza kuwa wanaendelea na jitihada za kutoa elimu kwa wananchi ili kujenga uelewa wa namna ya kuepukana na vitendo hivyo.



Lina Humphrey mkulima wa zao la stroberi akiendelea na shughuli za uvunaji wa zao hilo jana kwenye shamba lake lililoko Kata ya Nsalaga jijini Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wamiliki dhahabu waiangukia serikali kujengewa maabara

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

WAMILIKI wa viwanda vya kuchenjua dhahabu wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, bado wameendelea kuiangukia serikali kuwajengea maabara ya kisasa yenye uwezo wa kubaini wingi wa dhahabu kwenye udongo kabla ya kuchenjuliwa ili iwasaidie kuepuka hasara na kutoaminiana baina yao na wachimbaji wa madini.

Ombi hilo limetolewa mwishoni wa wiki na Hamis Rajab, kuwa uwapo wa maabara hiyo utasaidia kuongeza kasi ya uchimbaji wa dhahabu na kuongeza wigo wa ajira kwa wananchi wa Chunya.

"Uwapo wa maabara hiyo kutasaidia kupunguza malalamiko kwa wafanyabiashara wadogo wanaouza dhahabu kwenye vituo maalumu vya kuuzia bidhaa hizo," alisema Rajab.

Alisema kiwanda chake kimeajiri vijana 21 ambao wamekuwa msaada kwa familia yao na kujiepusha na vitendo mbalimbali vya uhalifu ikiwamo wizi na uvutaji bangi.

Alisema kikwazo kikubwa ni ukosefu wa maabara hiyo ambayo ingerahisisha shughuli za uchimbaji kwa sababu wachimbaji wasingetumia nguvu kubwa kutafuta madini kwenye mashimo marefu na makubwa badala yake kifaa hicho kingetumika kujua ubora na uhakika wa dhahabu yenyewe.

Mbunge wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka, alisema shughuli kubwa ya uzalishaji mali wilayani Chunya ni dhahabu na kwamba wanahitaji kuwekewa mazingira rafiki kwao ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo.

Alisema wachimbaji na wamiliki wa madini ya dhahabu kwa muda mrefu wamekuwa na uhitaji wa maabara ya kisasa kwa ajili kubaini wingi wa dhahabu kwenye udongo ili kupunguza matumizi makubwa ya nguvu na kemikali ambazo zina madhara kwa afya ya binadamu.

Alisema mara kadhaa ombi hilo aliliwasilisha kwenye vikao vya bunge na kwamba kinachosubiriwa ni utekelezaji wa suala hilo ili wamiliki wa migodi waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

# Chunya yatenga ekari 20,000 kilimo cha korosho

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, imetenga zaidi ya ekari 20,000 kwa ajili ya kilimo cha zao la korosho na kwamba vijana ndio walengwa wakuu katika uwekezaji wa kilimo hicho kwa ajili ya kutekeleza ajenda ya 10/30.

Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho nchini (CBT), Francis Alfred, alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu mikakati ya bodi hiyo katika kuhakikisha zao la korosho linakuwa miongoni mwa mazao muhimu mkoani Mbeya.

Alisema kwa sasa wamepata eneo wilayani Chunya kwa ajili ya kilimo hicho na wamelenga kuwasaidia vijana kujikita kwenye kilimo hicho ili kujikwamua na umaskini.

Alisema wamepanga kuhamasisha kilimo cha pamoja ili kupata mavuno mengi kufikia ajenda ya 10/30 na kuboresha maisha ya wakulima.

"Kwa sasa tunahamasisha kilimo cha pamoja ambapo ekari hizo zote zitalimwa na tutawapatia mbegu bora wakulima ambazo ni bora zenye mavuno mengi na tunaamini zitakidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi," alisema Alfred.

Aliongeza kuwa msimu uliopita wa kilimo walizalisha miche milioni 15 na msimu huu wamepanga kuzalisha zaidi ili kupata mavuno tani 700,000 na kuwafikia wakulima wasiopungua 300,000.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za kulevya nchini, Gerald Kusaya, alisema ili kufanikisha mipango ya Bodi ya Korosho nchini lazima wafanya uchunguzi wa kutosha ili kutekeleza masuala waliyojiwekea.

Alisema bodi hiyo inaonesha nia yake ya dhati katika kuwasaidia wakulima na wakiwa na dhamira ya dhati watafanikisha mpango huo na kuwasaidia wakulima wengi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Hata hivyo, aliitaka bodi hiyo kuongeza kasi ya usambazaji wa miche ya korosho kwa wakulima kwenye maeneo yote nchini kuwawezesha kupanda kwa wakati ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.





# Wasimamishwa kazi madai upotevu wa mil. 709/-

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATENDAJI wawili wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), wamesimamishwa kazi kutokana na madai ya upotevu wa mapato ya serikali Sh. milioni 709.

Akitoa taarifa ka waandishi wa habari juzi mjini hapo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Saada Mkuya Salum, aliwataja wafanyakazi hao kuwa ni Abdultif Abdalla Waziri, mfanyakazi wa Idara ya TEHAMA na Kassim Idrissa Mussa, wanaodaiwa kuchezea mfumo wa mapato kwa muda mrefu.

Waziri Mkuya alimtaka Kamishna wa Bodi hiyo kufuata utaratibu wa utumishi wa umma kuhakikisha wanakwenda katika mkondo wa sheria na kuitaka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), kuchunguza kwa muda mfupi tuhuma hizo ili sheria ichukue mkondo wake.

Pia, alimwagiza kamishna wa bodi hiyo kutumia taratibu za kiutumishi kuwasimamisha kazi watumishi wengine ambao ni wakuu wa idara za TEHAMA, Harith Abdul-aziz Ahmada, Mkuu wa Kitengo cha Madeni na Mapato, Asya Abdulsalam Hussein na Nassor Ali Juma, Meneja wa mifumo hiyo ZRB na kupelekwa ZAECA ili kufanyiwa uchunguzi dhidi ya tuhuma za upotevu wa fedha.

Alisema walibaini katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita kuna upotevu wa kodi unaotokana na wafanyabiashara na watendaji wa bodi hiyo ambao sio waaminifu.

Waziri Saada alisema wakati wanapitia mfumo huo kulikuwa kunaonesha kuna fedha inaoneakana kwenye mfumo kama imeingia, benki imelipwa na katika mfumo kuonekana risiti za benki kumbe watendaji wa ZRB ambao sio waaminifu wameingia kwenye mfumo huo na kufanya wanavyotaka wao.

Waziri Mkuya alisema kuna tuhuma nyingi za rushwa na wataendelea kuzifuatilia na yeyote atakayebainika kuhusika katika kadhia hiyo hatoachwa salama.

Naye Kamishna wa Bodi hiyo, Yussuf Juma Mwenda, alisema Februari 17, Rais Hussein Mwinyi, alipoitembelea ZRB katika mambo mengi aliyoyasema ni mifumo ya usimamizi wa kodi inachezewa kwa lengo la kukwepa kodi.

Aidha, alisema katika uchunguzi wao walibaini mfumo wa usimamizi wa kodi ukichezewa na kubaini baadhi ya watumishi wawili ambao sio waaminifu kwa kushirikiana na wafanyabiashara 20 katika kipindi cha Januari 2021 hadi Juni 2022.

Alisema kuchezewa kwa mfumo wa kodi kumesababisha upotevu wa mapato ya Sh. milioni 709 yakijumuisha mapato ya msingi na adhabu kitendo ambacho ni kinyume na maadili.




Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, akizungumza na wajasiriamali walioshiriki kongamano lililoandaliwa na Taasisi ya Rafiki wa Wanawake na Watoto Zanzibar wakati akizindua kongamano hilo katika ukumbi wa CCM Mkoa wa Amani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ kuendelea kusapoti vikundi vya wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuwa pamoja na vikundi vya wajasiriamali ili kuzifikia fursa zilizoko nchini kwa kuwainua wananchi wake.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo jana kwenye hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, katika ufunguzi wa kongamano la wajasiriamali lililoandaliwa na Taasisi ya Rafiki wa Wanawake na Watoto Zanzibar (RAWWAZA), lililofanyika, mjini hapo.

Alisema serikali imeanzisha programu maalum ya kuimarisha uwezeshaji wananchi kwa kengo la kutoa fursa za ajira kwa kuwawekea mazingira mazuri na kuwajengea uwezo vijana na wanawake ili kupunguza umaskini wa kipato.

Alisema serikali imeanzisha ujenzi wa mradi wa vituo vya kulea na kukuza wajasiriamali, mradi wa ujenzi wa vituo vya kutoa huduma za ujasiriamali na biashara pamoja na mradi wa ujenzi wa vituo jumuishi vya wajasiriamali.

Aidha, alisema serikali imejipanga kujenga masoko ya kisasa ambayo yatatoa nafasi kwa wajasiriamali kufanya shughuli zao za kiuchumi na kuchangamkia fursa za kuuza bidhaa wanazozalisha katika soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema kupitia fedha za ahuweni za UVIKO-19 serikali ilitenga Sh. bilioni 31.6 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupata mikopo yenye gaharama nafuu, boti na vifaa mbalimbali vya kuendesha shughuli zao.

Kwa upande wake Mwenyekiti RAWWAZA, Tawhida Cassian Galos, alisema taasisi hiyo imeanzishwa kwa lengo la kuunga mkono juhudi za serikali kuwasaidia wajasiriamali wa Zanzibar.

Aliishukuru serikali kutenga fedha nyingi za mikopo nafuu kwa wajasiriamali itakayowainua wanawake na vijana.

# Asasi kushirikiana na serikali kudumisha amani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kutatua migogoro na kuimarisha amani ya nchi, asasi za kiraia zimesema zitaendelea kushirikiana na serikali ili amani na utulivu wa nchi uendelee kutawala.

Mkurugenzi Msaidizi wa mradi wa Amani yetu Mshikamano Wetu, Jamila Juma Mahmoud, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, mjini hapo.

Alisema, katika kuhakikisha amani inaendelea kutawala nchini taasisi zisizo za kiserikali chini ya mradi huo ikiwamo Konrad Adenauer Stiftung (KAS) Tanzania na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) zimeandaa mafunzo kwa walengwa wakiwamo vijana na wanawake kutoka vyama vya siasa njia ya kutatua migogoro na kulinda amani.

Aidha, alisema kwa ushirikiano mzuri kati ya wadau mbalimbali wa mradi huo ikiwamo serikali, vyama vya siasa vilivyoteuliwa katika mradi huo na ofisi ya wakuu wa mkoa na wilaya wamepata mafanikio makubwa Unguja na Pemba.

Alisema miongoni mwa mafanikio hayo ni maridhiano ya kisiasa ambayo yamechangia kuzika tofauti na uhasama wa kisiasa ambazo zilisababisha chuki miongoni mwa Wazanzibari.

Jamila ambaye ni Mkurugenzi wa ZAFELA, alisema mradi huo umeweka mkazo kuhakikisha jamii ya Zanzibar hasa vyama vya siasa, vinafanya shughuli za kisiasa na kuwa na mikakati ya kutatua tofauti zao za kisiasa na kijamii kwa njia ya amani.

Naye kiongozi wa mradi huo, Maria Kayombo, alisema njia ambazo zimetumika na kuleta tija katika awamu iliyopita ni kufanya utafiti wa awali kama timu na kufanya shughuli zao zinazoendelea na kuwatumia wataalamu mbalimbali kuandaa dodoso elekezi ambayo wameitumia kufundishia vijana na wanawake.

Pia alisema waliandaa vipeperushi vyenye ujumbe mfupi na kueleweka kwa kila mmoja kwa urahisi pamoja na vikao vya mara kwa mara na kuwakutanisha makundi tofauti ya wanasiasa wenye vyama tofauti na kukaa pamoja.

Alisema hadi sasa kuna asasi za kiraia nane ambazo wanatarajia kuzipatia mafunzo na viongozi wa dini zote ili kuwapa elimu kama wanavyotoa kwa viongozi wa siasa ili kupanua wigo wa kuwajengea uwezo katika mradi huo kwa kuzingatia viongozi wa dini wana mchango mkubwa katika kuhakikisha wananchi wanaishi kwa utulivu.

Kwa upande wake, Mratibu wa mradi huyo 'Amani yetu, Mshikamano wetu' Almas Ali, alisema kero zilizojitokeza katika mradi huo ni baadhi ya wanasiasa wakibabaisha na kutojulikana wanatoka vyama gani.

"Changamoto zilizojitokeza hazikusababisha mradi kutoendelea, lakini ni ndogo sote tunafahamu kwamba kuna vyama vya siasa vimepita katika mpito kwa mfano CUF wamekuja katika vikao, lakini huwezi kumjua wanasema ni CUF sio wanachama wa CUF hivyo wanakuja pale na wanagombana hivyo tukawa tunawatumia viongozi wao watuletee," alisema Almasi.

Alisema changamoto zingine ni hofu ya washiriki wa mkutano ambao ni viongozi wa vyama tofauti kukaa pamoja hivyo ni wa ngazi za chini wanakubaliana pale walipopata elimu, lakini bahati mbaya huwa wanahofu ya yale waliokubaliana na kufanyiwa kazi na viongozi wao.

Almasi alisema matarajio ya wananchi wanaopewa elimu huwa ni makubwa ambayo kama vile huwa kuna hofu ya kutofikiwa matarajio hayo kwenye ngazi za juu taifa.

Mradi huo unategemewa kukamilika mwezi Februari, 2023, mbali na kujenga uwezo wa makundi, utakuwa na midahalo ya mara kwa mara kati ya watendaji wa kisiasa na wananchi kupitia vipindi vya redio na majadiliano.

# WAWATA yachukizwa utoaji mimba mabinti

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

CHAMA cha Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA), wameeleza kuchukizwa na vitendo vilivyokithiri vya utoaji mimba holela kwa mabinti.

Mwenyekiti wa WAWATA Taifa, Evaline Ntenga, alibainisha hayo juzi mkoani Shinyanga, wakati akizungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 50 ya chama hicho tangu kuanzishwa kwake mwaka 1972, sherehe zilizofanyika Kanisa Katoliki Parokia ya Ngokolo.

Alisema kazi ya WAWATA ni utume pamoja na kukemea mambo maovu ambayo yamekuwa yakifanyika ndani ya jamii, likiwamo suala la utoaji mimba holela kwa mabinti.

"Kinamama wenzangu nawaombeni tusimamie sana maadili ya watoto wetu, tunajua mko bize na maisha, lakini kuweni karibu na mabinti zenu, wapeni hata elimu ya kutumia njia asili za uzazi wa mpango, tunawatoa mimba sana watoto wetu ardhi hii inatulilia," alisema Ntenga.

Naye Katibu wa Chama cha Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA), Jimbo la Shinyanga, Beatrice Nangale, alitaja majukumu yao kuwa mbali na kuwakutanisha wanawake Wakatoliki kuwa pamoja, pia hupinga mapenzi ya jinsia moja, dawa za kulevya, uharibifu wa mazingira, utoaji mimba na mauaji ya vikongwe.

Aidha, alitaja shughuli zingine wanazozifanya za kiuchumi kuwa ni uuzaji wa vitenge vya WAWATA, huku akibainisha vikwazo ambavyo wamekuwa wakikutana navyo wakati wa utoaji elimu ndani ya jamii, kuwa ni mila, desturi pamoja na imani potofu hasa kwenye masuala ya ndoa.

Kwa upande wake, mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Gaudensia Kabaka, alipongeza kuanzishwa kwa chama hicho na kuwasihi waendelee kutoa elimu kwa jamii ili waishi kwa amani, upendo na kuacha vitendo viovu.



Meneja wa Benki ya NMB (Kanda ya Magharibi), Sospeter Magesse, akitoa maelezo kwa wanachama wa klabu ya biashara ya benki hiyo wa Wilaya ya Kasulu na Kibondo kuhusu matumizi ya simu na kadi za kielektroniki zinavyotumika kufanya miamala na huduma za kifedha ikiwamo mikopo inayotolewa na benki na manufaa ya huduma hiyo kwa wateja. Benki ya NMB ilikutana na zaidi ya wafanyabiashara 1,400 wa kanda hiyo ili kuwapa elimu ya biashara, mikopo na bima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waonywa ufichaji taarifa za uhamiaji sensa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wametakiwa kutokuficha taarifa za uhamiaji wa makazi wakati wa Sensa ya Watu na Makazi inayofanyika Agosti 23, mwaka huu na kutakiwa waonyeshe ushirikiano.

Mkufunzi kiongozi wa Sensa ya Watu na Makazi kutoka halmashauri hiyo, Mwalimu Chamo Mashauri, aliyabainisha hayo jana wakati wa tamasha la uhamasishaji wa sensa lililofanyika Kijiji cha Busenda, Kata ya Chona kwa kuandaliwa na Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani.

Alisema, kila mkazi wa Halmashauri ya Ushetu, atakiwa kutokuficha taarifa za uhamiaji, ulemavu, elimu, umiliki wa ardhi, majengo na kwa mtu atakayeondoka nyumbani siku ya tarehe hiyo ahakikishe anaacha taarifa muhimu za kutosha ili asije kukwamisha zoezi hilo.

Alitaja baadhi ya vilelezo vitakavyohitajika siku hiyo kuwa ni pamoja na taarifa za uzazi kwa wanawake wenye miaka 10 na kuendelea, na vifo vinavyotokana na uzazi vilivyotokea ndani ya siku 40 baada ya kujifungua na vitambulisho vya uraia au makazi.

Mashauri alisema, wakati wa utekelezaji wa sensa, makalani wataongozana na viongozi wa eneo husika na kuwataka viongozi hao kuwapatia fursa makarani kufanyakazi yao bila kuwaingilia kwasababu kishikwambia kitachotumika kuchukua taarifa kitakuwa na ramani ya eneo analopita.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Sophia Mjema alisema, hamasa ya kuwahamasisha wananchi kushiriki sensa ilianza tangu serikali ilipotangaza tarehe ya sensa, anamatumaini wananchi wote watashiriki kikamilifu na hawataficha taarifa zinazohitajika siku hiyo.

Alisema, kila mmoja ana haki ya kuhesabiwa siku ya tarehe hiyo na kuwasihi kutowaficha watoto wenye ulemavu kwa kuwa suala hilo limekuwa janga la taifa na kufanya hivyo ni kwenda kinyume na haki za binadamu na mtu anaweza kushtakiwa na kuchukuliwa hatua kama wahalifu wengine.

Kwa upande wake, Mbunge wa Ushetu, Emmanel Cherehani, alisema hamasa ya kushiriki sensa ya watu na makazi imekuwa ikifanyika mara kwa mara kupitia mikutano yake inayoendelea jimboni na kupitia vikao vya maendeleo ya kata wajumbe wamekuwa wakisisitizwa kufanya hivyo.

Alisema, hata lengo la kuanzisha tamasha hilo katika Kijiji cha Busenda, Kata ya Chona ni kuhamasisha wananchi kujitokeza kushiriki kikamilifu sensa ya watu na makazi na kuwambusha kutokuficha taarifa muhimu zinazohitajika na makarani wa sensa.

Mkazi wa kijiji hicho, Sondotuma Masanja alisema, kwenye familia yake ana mtoto mwenye ulemavu wa viungo atahakikisha anahesabiwa kama walivyo watu wengine.

Amri Juma alisema, ili serikali itenge bajeti inayotosheleza mahitaji ya wananchi wake, inahitaji kupata takwimu sahihi za idadi ya wananchi nchi nzima na anaendelea kutoa elimu ya sensa kwa majirani zake kwa kuwa ameshiriki mara kadhaa na faida yake anaifahamu vyema.

## Ma-DC, ma-DED waagizwa kutenga maeneo kilimo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI mkoani Shinyanga, imewaagiza wakurugenzi wa halmashauri sita za mkoa huo kwa kushirikiana na wakuu wa wilaya, kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya kilimo cha pamoja yatakayotumika kuwaelimisha wakulima namna ya kulima kisasa mazao ya chakula na biashara.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Sophia Mjema, alitoa agizo hilo jana akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Busenda, Kata ya Chona, Halmashauri ya Ushetu katika tamasha la uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi, lililoandaliwa na Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani.

Alisema, lengo la uanzishaji wa mashamba hayo ni moja ya utatuzi wa ajira kwa vijana watakaohitimu masomo yao, ule muda wa kukaa vijiweni au majumbani wakisubiri kuajiriwa na serikali watautumia kulima mazao ya chakula na biashara yakiwamo tumbaku, pamba na choroko.

Dk. Mjema alidai, baadhi ya vijana waliohitimu elimu ya kilimo na mifugo wanakosa mahala sahihi pa kuonyesha ujuzi wao na maeneo hayo yatawafanya kujiajiri kupitia kilimo kwa sababu pia pembejeo zimeshuka bei kutoka Sh. 131,676 hadi 70,000 kwa mbolea ya kukuzia ya DAP.

Aliwataka wakulima wanapovuna mazao yao, kuhakikisha wanatunza chakula na kuuza sehemu ya mazao ili kuondokana na njaa ndani ya familia kwa kuwa watakapouza chakula chote na kutegemea vilivyopo sokoni siku zote huwa ni vigumu kumudu gharama.

Pia, Mjema alisema, msimu uliopita Mkoa wa Shinyanga ulizalisha chakula kingi cha kutosha ikwamo mahindi, mpunga na choroko na kuwataka vijana kujikita katika kilimo na kuachana kushinda kwenye vijiwe.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani alisema, kwa kushirikiana na Mkurugenzi wake na madiwani, wanatarajia kutenga eneo zaidi ya hekta 30,000 za kilimo cha pamoja ambalo litatumika na vijana na utoaji wa elimu ya kulima kisasa kwa ajili ya kuongeza mavuno kwa wakulima.

Alisema, halmashauri hiyo inatarajia kupokea Sh. bilioni 28 kwa ajili ya kilimo na kila mkulima atahakikisha ananufaika na fedha hizo.

## Mafuriko yaua 50 Sudan

**KAHARTOUM,** Sudan

MAFURIKO yaliyosababishwa na mvua za msimu wa masika nchini Sudan, yamesababisha vifo vya watu 50 na kuharibu nyumba 8,170.

Msemaji wa kitengo cha taifa cha kuwalinda raia nchini Sudan, Brigedia Jenerali, Abdul-Jalil Abdul-Rahim alisema vifo 19 vimetokea jimbo la Kordofan Kaskazini, ikifuatiwa na jimbo la Mto Nile ambalo limerekodi vifo sana.

Hata hivyo hakusema lini vifo hivyo vimetokea.

Lakini msimu wa mvua nchini humo kwa kawaida unaanzia Juni hadi Septemba na mafuriko yanakuwa ya kiwango cha juu katika miezi ya Agosti na Septemba. **DW**



## Mwanamageuzi apandishwa kizimbani

**TEHRAN,** Iran

VYOMBO vya habari nchini Iran vimeripoti kwamba, Iran imemfungulia mashtaka mwanasiasa mwanamageuzi Mostafa Tajzadeh, ambaye aliwahi kufungwa na kukamatwa tena mwezi uliopita akituhumiwa kuhujumu usalama wa taifa.

Duru zilieleza Tajzadeh mwenye umri wa maka 65 ambaye mwaka jana aliingia katika mchakato wa kuwania urais bila mafanikio alifikishwa mahakamani mjini Tehran juzi.



Mwanasiasa huyo (pichani)aliwahi kuwa naibu waziri wa mambo ya ndani katika kipindi cha miaka ya 1997-2005 wakati wa utawala wa rais mwanamageuzi, Mohammad Khatami.

Alitiwa mbaroni mwaka 2009 wakati wa maandamano ya kupinga kuchaguliwa tena kwa rais wa wakati huo Mahmud Ahmadinejad. **DW**

# IEBC yafikia kuhakiki nusu kura, Odinga aonekana kuongoza

**NAIROBI,** Kenya

WAKATI Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya (IEBC) imefikia nusu ya ujumuishaji na uhakiki wa kura za urais, matokeo rasmi yaliyotangazwa yanaonesha mwanasiasa mkongwe, Raila Odinga, anaongoza.

Kwa mujibu wa matokeo yaliyowekwa kwenye ubao wa IEBC katika ukumbi wa Bomas jijini Nairobi, Odinga alikuwa na asilimia 54 ya kura mbele ya Naibu Rais William Ruto mwenye asilimia 45 kufikia mchana.

Kenya inayoongoza kwa kuwa na uchumi mkubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki na demokrasia inayoshamiri, ilifanya uchaguzi wa urais, ubunge na ugavana Agosti 9 mwaka huu.

Ruto na Odinga wanaonekana kuchuana kwenye kinyang'anyiro cha kumrithi Rais Uhuru Kenyatta, ambaye ametimiza ukomo wa mihula miwili madarakani.

Kenyatta alikosana na aliyekuwa mshirika na naibu wake, Ruto, mara tu ya uchaguzi wa mwisho wa mwaka 2017 na tangu hapo amekuwa akimsogeza Odinga karibu yake na hatimaye kumuunga mkono kwenye uchaguzi huu.

**Mawakala kwenye zoezi hili hawawezi kusonga mbele ni kama kwamba tunafanya ukaguzi wa kijasusi," aliwaambia waandishi wa habari.**

#### MATOKEO YAZUSHA WASIWASI

Jinsi utangazaji rasmi wa matokeo unavyosuasua umeibua wasiwasi miongoni mwa wananchi.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa IEBC, Wafula Chebukati, aliwakosowa mawakala wa vyama vya siasa, ambao wanaruhusiwa kuzichuja fomu za matokeo kabla ya kuwekwa kwenye majumuisho ya mwisho kusababisha ucheleweshaji huo.

"Mawakala kwenye zoezi hili hawawezi kusonga mbele ni kama kwamba tunafanya ukaguzi wa kijasusi," aliwaambia waandishi wa habari.

"Hatwendi mbele kwa haraka kama tunavyotakiwa. Zoezi hili linapaswa kukamilika haraka iwezekanavyo." Aliongeza.

Wawakilishi kutoka miungano ya Odinga na Ruto hawakupatikana mara moja kuzungumzia hali inavyoendelea.

Shirika la habari la Reuters na vyombo vingine vya habari vimekuwa vikijumuisha fomu za matokeo kutoka majimbo 291 zilizowekwa kwenye tovuti ya tume ya uchaguzi.

Hata hivyo, matokeo hayo bado hayajathibitishwa ingawa ujumuishaji wake unakwenda vyema na uko mbele ya ule wa matokeo rasmi ya IEBC.

#### MATOKEO YALIYOKUSANYWA NA REUTERS

Kufikia saa 3:00 usiku, Reuters ilikuwa imeshajumuisha fomu 241 zilizomwonesha Ruto akiongoza kwa takribani asilimia 52.3 ikilinganishwa na 47 za Odinga, huku wagombea wengine wawili wakiwa na chini ya moja baina yao.

Fomu nyingine 30 hazikuweza kujumuishwa kwenye matokeo hayo kwa sababu zilikuwa ama hazisomeki au zilikosa baadhi ya taarifa muhimu kama vile sahihi, majina ya majimbo au jumla kuu ya kura.

Fomu zinazojumuishwa na Reuters ni za awali na matokeo yake yanaweza kubadilika wakati wowote.

Kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi ya Kenya, baada ya fomu kuwekwa kwenye tovuti ya tume ya uchaguzi, zinatakiwa pia ziwasilishwe moja kwa moja kwenye kituo kikuu cha majumuisho, ambako wawakilishi wa vyama wanaweza kuzihakiki kuona endapo hazina mapungufu yoyote.

#### UGUMU WA KAZI YA KUJUMUISHA

Mchakato huu uliwekwa kwa lengo la kuzuwia malalamiko ya wizi wa kura ambayo yamewahi kuchochea ghasia kwenye chaguzi zilizopita.

Mgombea anayestahili kutangazwa mshindi wa urais lazima apate zaidi ya asilimia 50 ya kura za nchi nzima na asilimia 25 ya kura kutoka kwenye kaunti 24 kati ya 47. **DW**



Mlipuko uliosababishwa na shambulizi la bomu kutoka ndege za Israel katika mji wa Gaza baada ya kuibuka kwa mapigano kati ya vikosi vya nchi hiyo na wanamgambo wa Palestina. **PICHA: REUTERS**

# Ukraine yawalenga wanaotishia usalama kinu cha nyuklia

**KYIV,** Ukraine

UKRAINE imesema inawalenga wanajeshi wa Russia ambao wanaelezwa kukishambulia kwa risasi kinu kikubwa kabisa cha nyuklia barani ulaya au kukitumia kama ngome yao ya kijeshi kwa kuanzisha mashambulizi.

Hayo yanafanyika katika kipindi ambacho kundi la nchi saba tajiri duniani la G7 likiwa na hofu ya kutokea janga na kuitaka serikali ya Russia kuyaondoa majeshi yake katika eneo hilo la Zaporizhzhya.

Katika hotuba yake ya jana jioni, Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy alisema kila mwanajeshi wa Russia ambaye atalenga eneo la kinu hicho au kutumia eneo hilo kama ngao ya kujikinga lazima atambue kuwa atakuwa anasakwa na mawakala wa ujasusi wa Ukraine.

Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, ambalo lipo katika jitihada za kufanikisha ukaguzi wa eneo hilo limeonya kutokea janga la nyuklia endapo mapigano hayatasimamishwa. **DW**

# NBC YADHAMIRIA KUKUZA SEKTA MICHEZO, SANAA NA UTAMADUNI

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imesisitiza kuhusu dhamira yake ya kukuza na kuendeleza sekta ya michezo nchini kwa kuunga mkono jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali pamoja na wadau wengine wa sekta hiyo inayokua kwa kasi.

Akizungumza kwenye hafla ya jioni iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam ikilenga kuwapongeza na kuwakaribisha wanamichezo wa Kitanzania walioshiriki kwenye Mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika hivi karibuni mjini Birmingham nchini Uingereza, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema Sekta ya Michezo, Sanaa na Utamaduni ina mchango muhimu katika suala zima la ajira pamoja na kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na pato la taifa kwa ujumla.

**"Pamoja na kuitikia wito wa serikali katika kuinua sekta hii muhimu, Benki ya NBC tumebaini kwamba sekta hii ni eneo la kimkakati kiuchumi iwapo sisi kama wadau muhimu tutaiunga mkono," alisema Sabi kwenye hafla hiyo iliyohudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta hiyo wakiwamo viongozi waandamizi wa serikali wakiongozwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa.**

Sabi alibainisha kuwa benki hiyo ina dhamira ya dhati ya kushirikiana na wadau wa sekta ya michezo, sanaa na utamaduni na dhamira hiyo inapimwa kwa namna ambavyo taasisi hiyo inadhamini matukio mbalimbali ya kimichezo hapa nchini ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara (NBC Premier League), NBC Dodoma Marathon, mashindano ya mchezo wa gofu pamoja na kuunga mkono jitihada za ujenzi wa miundombinu ya michezo ikiwamo ujenzi wa viwanja vya mpira katika maeneo mbalimbali nchini.

"Hivyo basi, kwetu NBC milango ipo wazi kwa wadau mbalimbali wa sekta ya michezo, sanaa na burudani ili tuweze kushirikiana katika kukuza sekta hii muhimu, lengo likiwa ni kukuza ajira ambayo ni nyenzo muhimu kiuchumi na ustawi wa sekta ya fedha nchini," alisema.

Pamoja na kuwapongeza na kuwakaribisha wanamichezo wa Kitanzania walioshiriki kwenye Mashindano ya Jumuiya ya Madola, hafla hiyo pia ilihusisha makabidhiano ya taarifa ya namna bora ya kusimamia HAKIMILIKI na ugawaji wa Mirabaha kwa wamiliki wa kazi za sanaa nchini.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), akisalimiana na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, katika hafla iliyolenga kuwapongeza na kuwakaribisha wanamichezo wa Kitanzania walioshiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika hivi karibuni mjini Birmingham, Uingereza. Hafla hiyo iliandaliwa kwa ushirikiano na Benki ya NBC na kufanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wengine ni Ofisa Mkuu wa Uendeshaji benki hiyo, Alelio Lowassa (wa pili kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa NBC, Godwin Semunyu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kocha Dodoma Jiji ataka soka la kasi

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Dodoma Jiji FC kesho ikishuka katika Uwanja wa Jamhuri kuikaribisha Mbeya City katika mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu Bara msimu wa 2022/23 , Kocha Mkuu wa timu hiyo, Masoud Djuma, amesema kwenye mfumo wake anahitaji soka la kasi, ambalo anatakiwa awe na wachezaji wenye mbio, wanaokokota mpira kwenda mbele zaidi na uwezo wa kukaa na mpira.

Masoud, kocha wa zamani wa Simba, raia wa Burundi, amesema hiyo ndiyo sababu iliyomfanya kuondoa wachezaji wengi kwenye kikosi hicho na kusajili wengine kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Nilikuja hapa nikakutana na wachezaji ambao hawaendani na mimi, lakini sikutaka kufanya chochote kwanza zaidi ya kuibakisha timu Ligi Kuu na kweli nikafanikiwa. Mimi kama kocha nilikuwa nataka niwe na mfumo wangu, lakini kwa wakati ule ilishindikana, ligi imeisha kwa hiyo lazima nilete wachezaji wanaoendana na mimi. "Napenda mpira wa 'spidi' kwenda mbele, wachezaji kuwa na uwezo wa kukaa na mpira, kwa hivyo nilipendekeza hivyo nipate wachezaji wa aina hiyo, lakini kwa uwezo wa klabu yetu, wasiwe wale wa gharama kubwa sana, lakini wenye uwezo ninaouhitaji," alisema Masoud.

Kocha huyo amewashukuru viongozi wa Dodoma Jiji kwa kumtekelezea alichokihitaji kwenye usajili kwa asilimia 98.

"Asilimia 98 nimehusika mwenyewe kuchagua wachezaji wa kusajili na viongozi wamenisaidia kwa asilimia mbili kwa sababu baadhi ya wachezaji mimi nilikuwa siwajui. Lengo msimu ujao ni kubadilisha kila kitu, nilichotaka kuondoa ni mazoea, kubadili mazoezi, kuna wachezaji wako pamoja kwa muda mrefu kiasi kwamba wanaona kawaida tu, kwa hiyo tunabadilisha, tumesajili wachezaji ambao ni wazuri na nina uhakika msimu ujao tutafanya vema," alisema.

Baadhi ya wachezaji waliosajiliwa ni Aron Kalambo aliyerejea kwenye timu hiyo, Muhsin Malima, Hassan Kessy, Salum Kihimbwa, Hassan Mwaterema, Mwana Kibuta, Rashid Chambo, Aman Kyata, Paul Peter.

# Dirisha usajili Ligi Z'bar kufungwa Jumamosi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

ZIKIWA zimebaki siku sita za kufungwa kwa dirisha la usajili na uhamisho kwa ajili ya msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar 2022/23, klabu mbalimbali zimeendelea kufanya usajili wa wachezaji.

Dirisha la usajili na uhamisho wa wachezaji Zanzibar linatarajiwa kufungwa Jumamosi majira ya saa sita kamili usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Bakari (pichani chini), alisema kamati ya mashindano itaendelea kuhakikisha inasimamia kanuni zake katika kipindi hiki cha kuanza msimu mpya ligi hiyo.

Alisema katika kipengele hiki cha usajili na uhamisho kwa miaka ya nyuma kilikuwa kinaleta tabu kwa wachezaji na hata klabu kushindwa kufanya usajili na uhamisho kwa mujibu wa kanuni hali iliyokuwa ikisababisha kuwapo kwa kesi nyingi za rufani za wachezaji katika ligi mbalimbali za Zanzibar.

Alisema tangu ZFF kuanza kutumia mfumo maalum wa usajili kwa njia ya mtandao changamoto hii ya rufani za wachezaji zimepungua kwa kiasi kikubwa katika ngazi ya mikoa na wilaya, lakini zimeondoka kabisa katika ngazi ya Taifa.

"Tupo katika wakati wa usajili na uhamisho, mpaka sasa hakuna kesi yoyote ambayo tumeipata juu ya utata wa uhamisho wa mchezaji yeyote, hii pia ni mafanikio, lakini miaka ya nyuma kipindi kama hiki cha usajili ingekuwa nikesi, tutaendelea kufuatilia kuhakikisha kanuni zinafuatwa ili kuondoa migogoro," alisema.

Aidha, alisema Kamati ya Mashindano ya ZFF, itaendelea kutoa elimu Kwa Kamati zinazosimamia mashindano ngazi za mikoa na wilaya kuhakikisha klabu zinahamisha wachezaji kwa mujibu wa kanuni zao ili kuepuka migogoro kipindi cha ligi.

Hata hivyo, aliipongeza Bodi ya Ligi Zanzibar (ZLB), kwa kusimamia vema shughuli zote za usajili na zile zinazohusu klabu kwa kuhakikisha maboresho makubwa yanafanyika kuelekea msimu mpya.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FOFANA NA CHELSEA FRESH

CHELSEA imefikia makubaliano ya maslahi binafsi na mlinzi wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 21, Wesley Fofana, lakini ofa zao mbili zilikataliwa na Leicester City, ambao wanataka zaidi ya pauni milioni 80. ***(Mail)***

### AUBAMEYANG AWANIWA

KIUNGO wa Uholanzi, Frenkie de Jong, 25, na mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang (33), pia wanaweza kutimkia Stamford Bridge, huku Chelsea wakiongoza mbio za kutaka kuwasajili wachezaji hao wa Barcelona. ***(Express)***

### MORATA ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imeanzisha mazungumzo na Atletico Madrid juu ya uwezekano wa kumsajili straika wa Hispania, Alvaro Morata, 29, ambaye ada yake ni pauni milioni 30. ***(Athletic, via Mail)***

### UNITED: RASHFORD HAUZWI

MANCHESTER United pia imeipasha Paris St-Germain kwamba, mshambuliaji wa kimataifa wa England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 24, hauzwi. ***(Mail on Sunday)***

### GALLAGHER AWINDWA

KLABU ya Newcastle imemfanya kiungo wa Chelsea na England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 22, kuwa chaguo lao namba moja kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili. ***(Sun)***

### CELSO HUYOOO VILLARREAL

KIUNGO wa Tottenham Hotspur, Giovani lo Celso, 26, yupo nchini Hispania kukamilisha uhamisho wa mkopo wa muda mrefu na Villarreal. ***(Fabrizio Romano)***

### GOMEZ SAFI CITY

MLINZI wa kushoto wa Anderlecht, Sergio Gomez, 21, tayari amejiunga na Manchester City huku ada yake ikitajwa kwamba ni pauni milioni 11 kwa mchezaji huyo raia wa Hispania. ***(Fabrizio Romano)***

### PEP AMTAKA TIERNEY

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anamwania mlinzi wa kushoto wa Arsenal, Kieran Tierney, 25, ili kuimarisha safu yake ya ulinzi. ***(Mail on Sunday)***

### RAMOS AWANIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United ipo kwenye mazungumzo na Benfica ili kufikia ofa ya pauni milioni 35 ya kumsajili straika wa Ureno, Goncalo Ramos, 21. ***(Sunday Express)***


### NDOMBELE NA NAPOLI

KIUNGO wa Tottenham Hotspur, Tanguy Ndombele, 25, amefikia makubaliano ya mkopo wa muda mrefu na Napoli. ***(Fabrizio Romano, via Sun)***

### FOREST KUMSAJILI MAUPAY

KLABU ya Nottingham Forest imefikia makubaliano ya kumsajili straika wa Brighton, Mfaransa Neal Maupay mwenye umri wa miaka 25, kwa pauni milioni 15. ***(Athletic)***

## DONDOO ZA MAGAZETI YA



# JESUS: ARSENAL HII TAMU SANA AISEE

**LONDON,** England

**Ninafanya mazoezi kila siku, mimi na Eddie (Nketiah) tukifanya kazi ya kumalizia, nadhani...**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Gabriel Jesus, amesema amefurahishwa na kikosi chake kuanza msimu huu vizuri kwenye Ligi Kuu England.

**'Washikabunduki' hao walipata ushindi wa pili mfululizo wakati walipoibuka na ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Leicester City kwenye Uwanja wa Emirates, Jumamosi.**

Mbrazil huyo alihusika katika mabao yote manne, akifunga mara mbili huku akisaidia pasi mbili za mabao, na alikiri baada ya mchezo huo kwamba, amefurahishwa zaidi na kiwango cha mwanzo mwa msimu huu cha 'Washikabunduki' hao.

"Nina furaha sana, si tu kwa sababu ya mabao yangu, lakini jinsi timu inavyocheza," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 akiiambia BBC Sport.

"Katika nyakati ngumu tuliruhusu mabao mawili, lakini tuliendelea kucheza vizuri na kujaribu kufunga.

"Tunajua sifa walizonazo. Wana wachezaji wengi wazuri, wanaokimbia nyuma, Jamie Vardy ni mmoja wa washambuliaji bora kwenye ligi.

"Nina furaha sana na pointi tatu. Ni muhimu."

Jesus alijiunga na Arsenal kwa kitita cha pauni milioni 45 akitokea Manchester City msimu wa majira ya joto.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil aliongeza kuwa anafurahia nafasi ya kuongoza safu ya ushambuliaji ya timu hiyo chini ya Mikel Arteta, akisema: "Ninaifurahia sana.

"Sio kwamba sikuwa na furaha kule City. Nilitaka tu kucheza. Nilielewa klabu na kocha, lakini wakati mwingine wachezaji wanataka tu kucheza.

"Ninafanya mazoezi kila siku, mimi na Eddie (Nketiah) tukifanya kazi ya kumalizia. Nadhani Arsenal ina washambuliaji wawili wazuri."

Arsenal itasafiri kumenyana na Bournemouth wikendi ijayo huku klabu hiyo ya Kaskazini mwa London ikitarajiwa kuendelea na mwanzo mzuri wa msimu wao kwa asilimia 100.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 315,

MECHI KALI
NAMUNGO
VERSUS
MTIBWA SUGAR
1 | 2.31
X | 2.70
2 | 3.65

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG AWAPONDA WACHEZAJI UNITED



**LONDON,** England


ERIK ten Hag amesema angeweza kuwatoa wachezaji wake wote "wenye kiwango duni" wakati wa mapumziko baada ya orodha ya makosa kuwaweka chini kwa mabao 4-0 kabla ya mapumziko dhidi ya Brentford, Jumamosi.

Katika kipindi cha kwanza cha kustaajabisha katika joto kali la magharibi mwa London, Manchester United walifanya mojawapo ya matokeo mabaya zaidi katika miaka 30 ya kucheza Ligi Kuu England - huku kikosi cha Ten Hag kilichojaa makosa kikiadhibiwa vibaya chini ya kocha wao huyo mpya.

Kipa David de Gea aliruhusu kombora rahisi la Josh Dasilva kutambaa chini ya mwili wake kwenye lango la karibu baada ya dakika 10 kabla ya pasi kumweka matatani mchezaji wa zamani wa Brentford, Christian Eriksen.

Cristiano Ronaldo - aliyerejeshwa kwenye kikosi cha kwanza - alipoteza nafasi tatu katika matokeo ambayo yanawaacha vijana hao wa Ten Hag mkiani mwa Ligi Kuu ya England wakiwa hawana pointi, huku Liverpool wakiwa ndio wapinzani wao wafuatao kucheza nao pale Old Trafford.

Alipoulizwa kuhusu kubadili kwake wachezaji watatu wakati wa mapumziko, jambo ambalo lilimfanya kuwatoa mabeki Lisandro Martinez na Luke Shaw pamoja na Fred, Ten Hag alisema: "Nilibadilisha watatu, lakini ningeweza kuwabadilisha wote.



## *Xavi ataka mashabiki kuwa wavumilivu*

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Xavi amewaomba mashabiki "wavumilie" baada ya timu yake kutoka suluhu na Rayo Vallecano katika mechi ya ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Wenyeji walitawala mpira, lakini walipoteza katika nafasi tatu za kufunga na walilenga goli mara sita pekee kati ya 21 walizojaribu, ingawa walishuhudia juhudi mbili zikiokolewa na mlinda mlango.

Hiyo imeifanya safu ya ushambuliaji ya Barcelona kuonekana kuwa butu kwenye LaLiga hadi mechi tatu bila bao au ushindi, kuanzia mwishoni mwa msimu uliopita ikiwa ni mara ya kwanza kwa klabu hiyo kuwa na msururu wa aina hiyo ya matokeo tangu Oktoba 2003.

Baada ya majuma kadhaa ya sintofahamu, klabu hiyo iliweza kusajili wachezaji wapya Robert Lewandowski, Raphinha, Andreas Christensen na Franck Kessie, ambao wote walicheza mechi yao ya kwanza kwenye sare hiyo.

Barca bado hawajamsajili Jules Kounde, aliyesajiliwa kutoka Sevilla, na wanaendelea kuhusishwa na kuongeza wachezaji wengine kabla ya dirisha la usajili kufungwa Septemba Mosi, mwaka huu huku Xavi akiwasihi mashabiki kuamini mchakato wa klabu hiyo.

## HABARI MICHEZO


# 715,520 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/08/22 | 19:00 | Rakow Czestochowa vs Slavia Prague | 2.73 | 3.24 | 2.53 |
| 02. 18/08/22 | 19:30 | El Gouna vs Ghazl EL Mahallah | 2.50 | 2.86 | 3.07 |
| 03. 18/08/22 | 19:30 | Al Masry Club vs Ismaily SC | 2.39 | 2.86 | 3.26 |
| 04. 18/08/22 | 20:00 | Pyunik Yerevan vs Sheriff Tiraspol | 2.83 | 3.13 | 2.52 |
| 05. 18/08/22 | 20:00 | Apollon Limassol vs Olympiakos | 3.37 | 3.22 | 2.16 |
| 06. 18/08/22 | 20:00 | CSKA Sofia vs FC Basel | 3.04 | 3.24 | 2.32 |
| 07. 18/08/22 | 20:00 | BSC Young Boys vs Anderlecht | 2.16 | 3.48 | 3.13 |
| 08. 18/08/22 | 20:00 | Maccabi Tel Aviv vs Nice | 3.02 | 3.22 | 2.33 |
| 09. 18/08/22 | 21:00 | HJK Helsinki vs Silkeborg | 2.87 | 3.22 | 2.43 |
| 10. 18/08/22 | 21:00 | SC Dnipro 1 vs AEK Larnaca | 2.63 | 3.23 | 2.63 |
| 11. 18/08/22 | 21:00 | Zrinjski Mostar vs Slovan Bratislava | 2.62 | 3.18 | 2.67 |
| 12. 18/08/22 | 21:15 | Maribor vs CFR Cluj | 3.03 | 3.13 | 2.38 |
| 13. 18/08/22 | 22:00 | Austria Vienna vs Fenerbahce | 2.78 | 3.29 | 2.46 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 15/08/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:45 | 5120 | Kelantan United FC vs Uitm FC | 1.74 | 3.47 | 4.21 |
| 12:00 | 5332 | Gangwon vs Suwon City | 2.07 | 3.30 | 3.20 |
| 13:00 | 5904 | Sangju Sangmu vs FC Seoul | 2.66 | 3.30 | 2.38 |
| 15:00 | 3718 | Tianjin Teda vs Changchun Yatai | 2.99 | 3.33 | 2.15 |
| 15:00 | 5359 | Hebei Zhongji vs Shandong Luneng | 26.43 | 8.61 | 1.06 |
| 17:00 | 1087 | Baalama vs AL Karmel | 1.58 | 3.62 | 5.29 |
| 17:25 | 5503 | Al-Sailiya SC vs Qatar SC | 2.56 | 3.20 | 2.51 |
| 17:30 | 4591 | Maritimo vs GD Chaves | 2.30 | 3.17 | 3.07 |
| 18:00 | 1890 | FK Radnicki 1923 vs Cukaricki St | 3.40 | 3.15 | 2.05 |
| 18:00 | 5564 | Hifk vs Seinajoen JK | 4.50 | 3.82 | 1.62 |
| 18:30 | 3222 | Athletic Bilbao vs Mallorca | 1.59 | 3.72 | 5.83 |
| 18:30 | 3895 | Real Oviedo vs FC Andorra | 1.67 | 3.39 | 5.39 |
| 19:00 | 1812 | Viljandi Tulevik vs Viimsi JK | 24.13 | 11.06 | 1.07 |
| 19:00 | 2126 | Adanaspor vs Tuzlaspor | 2.31 | 3.24 | 2.80 |
| 19:00 | 3879 | Ilves 2 vs Tampere United | 2.61 | 3.84 | 2.19 |
| 19:00 | 4119 | FC Nomme United vs Paide Linnameeskond | 2.68 | 3.94 | 2.26 |
| 19:00 | 4559 | Ruch Chorzow vs Chojnice | 1.92 | 3.29 | 3.64 |
| 19:00 | 4562 | Namungo vs Mtibwa Sugar | 2.31 | 2.70 | 3.65 |
| 19:15 | 5634 | Konyaspor vs Basaksehir | 2.71 | 3.36 | 2.45 |
| 19:30 | 1582 | Nancy vs Bourg Peronnas | 2.21 | 3.09 | 3.24 |
| 19:30 | 5488 | Verona vs Napoli | 3.36 | 3.41 | 2.05 |
| 19:30 | 5752 | Rubin Kazan vs Urozhay Krasnodar | 1.27 | 4.70 | 9.80 |
| 19:35 | 5902 | AL Wakrah vs Umm-Salal SC | 2.32 | 3.53 | 2.59 |
| 20:00 | 1704 | FC Arouca vs Gil Vicente | 2.60 | 3.26 | 2.60 |
| 20:00 | 1877 | BK Olympic vs IFK Malmo | 1.25 | 5.50 | 8.64 |
| 20:00 | 1962 | Aarhus vs Lyngby | 1.92 | 3.42 | 3.82 |
| 20:00 | 2511 | IK Brage vs Landskrona Bois | 1.78 | 3.77 | 4.28 |
| 20:00 | 2922 | BK Hacken vs Mjallby | 1.51 | 4.04 | 5.32 |
| 20:00 | 3148 | Brommapojkarna vs AFC Eskilstuna | 1.51 | 4.77 | 5.28 |
| 20:00 | 5807 | Korona Kielce vs Warta Poznan | 2.45 | 2.99 | 2.79 |
| 20:10 | 4153 | IFK Goteborg vs Hammarby | 3.55 | 3.45 | 1.89 |
| 20:30 | 3492 | Lugo vs Albacete Balompie | 2.15 | 3.09 | 3.44 |
| 20:30 | 4653 | Getafe vs Atletico Madrid | 4.45 | 2.98 | 1.96 |
| 21:00 | 1903 | Maastricht vs NAC Breda | 3.97 | 3.78 | 1.76 |
| 21:00 | 2278 | Jong PSV vs Dordrecht | 1.46 | 4.48 | 5.58 |
| 21:00 | 2954 | Jong Utrecht vs Heracles Almelo | 4.09 | 3.79 | 1.73 |
| 21:00 | 3592 | Erzurum BB vs Pendikspor | 2.00 | 3.44 | 3.24 |
| 21:00 | 4180 | Keflavik IF vs KR Reykjavik | 2.66 | 3.54 | 2.26 |
| 21:15 | 5294 | Olimpija Ljubljana vs ND Gorica | 1.40 | 4.31 | 6.47 |
| 21:45 | 2239 | Cork City vs Waterford Utd | 2.21 | 3.38 | 2.84 |
| 21:45 | 2980 | Juventus vs Sassuolo | 1.49 | 4.32 | 5.63 |
| 21:45 | 3716 | Kasimpasa vs Fenerbahce | 3.16 | 3.71 | 2.05 |
| 21:45 | 5657 | US Quevilly Rouen vs St Etienne | 3.65 | 3.25 | 2.01 |
| 22:00 | 4292 | Liverpool vs Crystal Palace | 1.19 | 6.19 | 12.98 |
| 22:15 | 3457 | Breidablik vs Vikingur Reykjavik | 1.91 | 3.68 | 3.28 |
| 22:15 | 4032 | Fram Reykjavik vs Leiknir | 1.95 | 3.59 | 3.25 |
| 22:30 | 1365 | Pacos Ferreira vs Portimonense | 2.36 | 3.12 | 3.02 |
| 22:30 | 3960 | Betis vs Elche | 1.44 | 4.43 | 6.65 |
| 22:30 | 5708 | Leixoes vs CD Trofense | 2.24 | 3.18 | 3.08 |
| 23:00 | 5921 | FC Cartagena vs Ponferradina | 2.15 | 3.26 | 3.26 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MPANGO AIPONGEZA CRDB KWA KUKUSANYA BIL.1/- KUSAIDIA JAMII

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa pongezi kwa mbio za hisani za kimataifa zinazoandaliwa na Benki ya CRDB, maarufu CRDB Bank Marathon, kwa kufikisha lengo la kukusanya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kusaidia jamii.

**Dk. Mpango alitoa pongezi hizo Dar es Salaam jana wakati akikabidhi mfano wa hundi kwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Hospitali ya CCBRT muda mfupi baada ya kukamilika kwa mbio hizo ambazo zilishirikisha zaidi ya wakimbiaji 6,200.**

Aidha, alipongeza uamuzi wa Benki ya CRDB kuendelea kusaidia upasuaji wa watoto wenye magonjwa ya moyo pamoja na wazo jipya la kusaidia upatikanaji wa huduma salama za uzazi kwa kinamama wenye ujauzito hatarishi.

"Afya ya mama na mtoto ni moja ya maeneo yanayopewa kipaumbele kikubwa katika sera ya afya. Ninafarijika kuona mbio hizi zinasaidia kuimarisha eneo hili kwa kufanikisha upatikanaji wa huduma ya matibabu kwa watoto na kinamama," alipongeza.

Dk. Mpango alisema fedha hizo zilizokusanywa, zitasaidia kupunguza makali ya gharama kwa ajili ya upasuaji wa moyo na huduma za uzazi kwa kinamama wenye ujauzito hatarishi, ambazo watu wengi hawawezi kuzimudu pamoja na serikali kutoa ruzuku ya asilimia 80.

Viongozi mbalimbali walifuatana na makamu wa rais kushiriki mbio hizo wakiwamo Rais mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Mussa Zungu, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekule, na Waziri wa Michezo Zanzibar, Tabia Mwita Maulid.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alibainisha kuwa mbizo za mwaka huu zimevuka lengo la ukusanyaji wa Sh. bilioni moja na kutoa shukrani kwa kampuni na taasisi zilizojitokeza kushirikiana na benki hiyo pamoja na wakimbiaji waliojitokeza kutoka ndani na nje ya nchi.

Nsekela aliwashukuru Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohammed Janabi na Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi kwa ushirikiano wao huku akiweka mkazo kuwa kaulimbiu ya benki hiyo isemayo 'Kasi Isambazayo Tabasamu', imefanikiwa kutokana na mchango wao wa dhati.

Katika mbio hizo washiriki takribani 60 waliofanya vizuri, walijishindia zawadi zenye jumla ya Sh. milioni 100. Zawadi hizo zinaifanya CRDB Bank Marathon kuwa mbio zinazolipa zaidi nchini ambapo washindi wa Km 42 kwa wanawake na wanaume waliondoka na kitita cha Sh. milioni 10 kila mmoja.

Akitangaza matokeo ya mbio hizo, Mkurugenzi wa Mawasiliano Benki ya CRDB, Tully Mwambapa, alisema kwa upande wa kilometa 42, Joseph Munywoki, raia wa Kenya ameibuka kinara akitumia muda wa 02:14:56, wakati Shoron Kosgei, raia wa Kenya aliibuka mshindi kwa upande wa wanawake akitumia muda 02:33:56.

Kwa mbio za kilometa 21, mshindi kwa upande wa wanaume alikuwa Samwel Mailu, raia wa Tanzania aliyetumia muda wa 01:02:04, kwa upande wa wanawake mshindi alikuwa Agnes Ngolo wa Tanzania aliyetuumia muda wa 01:09:16. Katika Km 10, mshindi kwa upande wa wanaume alikuwa Gabriel Geay, raia wa Zambia aliyetumia muda wa 00:28:16, kwa wanawake Maysellina Issa wa Tanzania alishika nafasi ya kwanza baada ya kutumia muda wa 00:33:52.

Katika mashindano ya mbio za baiskeli kilometa 65, Richard Laizer raia wa Tanzania aliibuka mshindi kwa upande wa wanaume akitumia muda wa 01:39:24, upande wa wanawake Julia Miringu raia wa Tanzania aliibuka mshindi baada ya kutumia muda wa 01:45:11.

Kati ya washiriki 6,200 walioshiriki katika CRDB Bank Marathon mwaka huu, asilimia 79 ni Watanzania, wakimbiaji wa kimataifa walioshiriki ni zaidi ya 1,300.




Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, akimkabidhi mshindi wa kwanza wa mbio za kilometa 42, Joseph Munywoki raia wa Kenya, hundi yenye thamani ya Sh. milioni 10 baada ya kuwashinda wenzake katika mbio za hisani za kimataifa za Benki ya CRDB "CRDB Bank Marathon" zilizokuwa na lengo la kukusanya Shilingi bilioni moja kwa ajili ya kusaidia jamii. Mbio hizo zilifanyika jana kwenye viwanja vya Farasi Oysterbay, Dar es Salaam. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Fountain Gate yaitaka Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Fountain Gate ya Morogoro inayojiandaa na Ligi ya Championship, imetaja mikakati na malengo yao ni kupanda na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/24.

Kocha msaidizi wa timu hiyo, Edward Lazaro, amesema mikakati yao kuanzia Bodi ya Klabu hiyo, viongozi, benchi la ufundi na wachezaji ni kuhakikisha wanaipandisha timu hiyo daraja.

"Tupo kambini kwa wiki tatu sasa hapa Morogoro tunajiandaa na Ligi ya Campionship, mikakati na malengo yetu ya pamoja wote kuanzia bodi, benchi na ufundi mpaka wachezaji ni kuipandisha timu daraja, na hilo linaonekana kwa sababu tuna wachezaji wazuri, makocha wazuri, viongozi safi, pamoja na kambi na huduma bora. Tunachofanya sisi ni kutengeneza muunganiko wa timu na tutahakikisha tunapata matokeo mazuri nyumbani pale kwenye Uwanja wa CCM Shabib, Gairo ndiyo utakuwa uwanja wetu wa nyumbani, lengo ni kupanda daraja na kuongeza timu kwenye mkoa wa Morogoro," alisema Lazaro.

Ligi ya Championship inatarajiwa kuanza Septemba 17, mwaka huu, ingawa mpaka sasa ratiba kamili haijatoka.

Michezo
Jumatatu Agosti 15, 2022
Nipashe



Jesus: Arsenal hii tamu sana UKURASA 21

# Nabi aing'ata sikio Simba kwa Zoran

## ●●● Atoa siri ya ushindi Ngao ya Jamii, Mayele naye...

**Na Saada Akida**

HUKU akitaja siri ya kupata matokeo chanya na kufanikiwa kutetea Ngao ya Jamii juzi, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesifu ubora wa kikosi cha Simba msimu huu akilinganisha na uliopita huku akitaka Kocha Zoran Maki apewe muda zaidi wakukisuka.

**Yanga iliichapa Simba mabao 2-1 katika mechi hiyo ya Ngao ya Jamii maalum kwa kuukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, shukran kwa Fiston Mayele aliyefunga mabao yote mawili huku lile la kufutia macho kwa Simba likifungwa na Pape Sakho.**

Akizungumza baada ya mchezo huo, Nabi alisema pamoja na ushindi huo, lakini kikosi cha Simba cha msimu huu ni bora ukilinganisha na kile cha msimu uliopita, hivyo wanachotakiwa ni kumpa muda kocha Zoran ili aweze kukiunganisha na kupandikiza falsafa zake.

Kuhusu siri ya ushindi, Nabi alisema kikubwa ni maandalizi mazuri waliyofanya na wachezaji kucheza kwa kujituma kuipigania timu yao.

"Niwapongeze wachezaji wangu, wamecheza vizuri hata tulipotanguliwa kufungwa hawakuhamaki, walitulia na kucheza vile tulivyowaelekeza hatimaye tukapata tulichokihitaji ambacho ni kutetea Ngao yetu ya Jamii," alisema Nabi.

Kocha huyo raia wa Tunisia, alisema pamoja na matokeo hayo, bado anaendelea kukisuka kikosi chake ili kiweze kucheza kwa kiwango cha juu zaidi ya kile walichokionyesha kwenye mchezo huo.

Kwa upande wake Kocha Mkuu wa Simba, Zoran alisema kilichosababisha kupoteza mchezo huo ni ubora waliokuwa nao wapinzani wao, Yanga.

Mserbia huyo alisema kipindi cha kwanza waliushika mchezo na kufanya mashambulizi kadhaa kwenye lango la wapinzani wao, lakini walikosa umakini kwenye kuzitumia nafasi.

"Kipindi cha pili ndicho kilikuwa kibaya zaidi kwetu, wapinzani walikuja juu na kutushambulia mfululizo na bao la mapema la kusawazisha lilituchanganya zaidi na kujikuta tunapoteza mchezo," alisema Zoran.

Aidha, Zoran amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana muda wote wa mchezo ingawa matokeo hayakuwa upande wao.

Naye muuaji aliyepeleka kilio Simba, Mayele amesema ushindi walioupata na kufanikiwa kutetea taji lao la Ngao ya Jamii, ni mwanzo mzuri wa kufikia malengo yao kwa msimu wa 2022/23 kwa kuendelea kufanya vizuri michezo iliyopo mbele yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mayele alisema ana matumaini makubwa timu hiyo itaendelea kutetea mataji yao yote mawili, yaliyobaki ambayo ni la Ligi Kuu Bara na Kombe la FA.

"Mchezo wa leo (juzi), ulikuwa na ushindani mkubwa sana, Simba kipindi cha kwanza walikuwa bora ila tulipokwenda mapumziko tulipewa maelekezo na hatimaye kutwaa taji, nina imani huu ni mwanzo mzuri katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Mayele.

Yanga itashuka dimbani ugenini kesho kuanza kutupa karata yao ya kwanza kwenye mbio za kutetea ubingwa wa Ligi Kuu itakapovaana na Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

TULIA WEWE...



Viungo wa Simba na Yanga, Jonas Mkude (kushoto) na Feisal Salum 'Fei Toto', wakizipambania timu zao kwenye mechi ya Ngao ya Jamii iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa Yanga kushinda mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Ligi Kuu Bara leo, makocha watamba

**Shufaa Lyimo na Cheji Bakari**

PAZIA la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23 litafunguliwa leo saa 10:00 jioni kwa timu nne kushuka dimbani ambapo timu iliyopanda daraja msimu huu, Ihefu itaikaribisha Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Highland Estate, Mbarali, Mbeya.

Mbali na mechi hiyo ya kwanza kabisa msimu huu, mechi nyingine itakayochezwa leo ni kati ya Namungo itakayokuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani Ilulu mkoani Lindi dhidi ya Mtibwa Sugar ambayo baada ya kuponea chupuchupu msimu uliopita, iliacha wachezaji zaidi ya 20 na kusajili wengine wapya.

Kuelekea mechi hizo za leo, timu ya Mtibwa Sugar imesema itamkosa mlinda mlango wake, Mohammed Makaka, ambaye aliumia mkono kwenye mchezo wa kirafiki walioucheza dhidi ya Fountain Gate Agosti 7, mwaka huu katika Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, daktari mkuu wa timu hiyo, Laurence Francis, alisema Makaka amepata jeraha kubwa hivyo atakaa nje kwa wiki nane.

"Makaka aliumia vibaya, tumemfanyia uchunguzi tukabaini amevunjika kiganja, hivyo atakaa wiki nane nje bila kujishughulisha na mpira mpaka hapo atakapokaa sawa," alisema Francis.

Kwa upande wake Kocha Mkuu wa timu hiyo, Salum Mayanga alisema licha ya kutambua utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa amejipanga vizuri kuwakabili wapinzani wao hao.

Kwingineko Kocha wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, amewataka mashabiki wa timu hiyo kujiandaa kupata matokeo mazuri katika michezo ya Ligi Kuu Bara msimu huu.

"Kutokana na usajili nilioufanya mwenyewe, naamini tutaleta changamoto kwa timu za Ligi Kuu msimu huu, wachezaji wote wapo salama na afya njema, hivyo Ruvu Shooting wajiandae kesho (leo)," alisema Katwila.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >